X,
Weds.
Jumatano

8


THUR
Alhamisi

1. Leo ni siku gani?

   Leo ni Jumatatu, siku ya kazi.

2. Kuna siku ngapi katika juma (wiki)?

   Kuna siku saba kwa kalenda yetu.

3. Waswahili wanataja siku za juma?

   Ndio, wanaanza na Ijumaa, siku ya kwanza.

4. Hiyo ni sikukuu kwa Waswahili?

   Ni sikukuu kwa Waislamu.

5. Wao wanaabudu Mungu siku hiyo?

   Ndio, na Wakristo wanaabudu Jumapili.

6. Siku za kazi ni kutoka Jumatatu hata Jumamosi?

   Ndio, ila kwa Waislamu.

7. Utasafiri kesho siku ya Jumanne?

   La, nitasafiri kesho kutwa, Jumatano.

8. Utarudi baada ya siku chache?

   Nitarudi siku ya Alhamisi.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Leo ni Jumatatu.
Leo ni Jumatatu.

Jumanne, Jumatano, Jumapili, Jumamosi.

b. Tunafanya kazi siku tano kwa wiki.
Tunafanya kazi siku tano kwa wiki.

sita, saba, mbili, tatu, nne.

c. Waswahili wanahesabu siku kutoka Ijumaa.
Waswahili wanahesabu siku kutoka Ijumaa.

sisi, hapa, yeye, ninyi.

d. Waislamu wanaabudu Ijumaa.
Waislamu wanaabudu Ijumaa.

sisi, hao, Isa, wewe.

e. Jumatatu ni siku ya kazi.
Jumatatu ni siku ya kazi.

leo, kesho, Alhamisi, Jumamosi.

f. Leo ni sikukuu kwa wote.
Leo ni sikukuu kwa wote.

kesho, Jumapili, kesho kutwa, Jumanne.

2. Substitution Drill

a. Jumatatu
-------- ni sikukuu.
Jumatatu ni sikukuu.

Alhamisi, Ijumaa, Jumapili, Jumamosi.

b. kesho

Tutaondoka ----- na tutafika kesho kutwa.
Tutaondoka kesho na tutafika kesho kutwa.

jioni, asubuhi, mapema, sasa.

c. Wanaabudu

--------- siku ya Jumapili.
Wanaabudu siku ya Jumapili.

pumzika, fanya kazi, cheza, lima.

d. wiki

Tutamaliza kazi ---- hii.
Tutamaliza kazi wiki hii.

siku, mwezi, mwaka, saa.

e. siku

Nitarudi baada ya ---- chache.
Nitarudi baada ya siku chache.

miezi, wiki, saa, dakika.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 31

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. Phonological target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the questions and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Leo ni siku gani?
2nd: Leo ni Jumapili.

kesho, kesho kutwa

b. 1st: Utakaa kule siku ngapi?
2nd: Nitakaa kule siku nne.

hapa, nyumbani, hospitali, Nairobi.

c. 1st: Kuna siku ngapi katika wiki?
2nd: Kuna siku saba.

mwezi huu, mwaka huu.

d. 1st: Wanaabudu siku gani?
2nd: Wanaabudu Ijumaa.

pumzika, fanya kazi, shindana, kwenda skuli.

e. 1st: Utasafiri kesho?
2nd: La, nitasafiri leo.

kesho kutwa, Jumapili, Alhamisi, Ijumaa.

5th PERIOD RECOMBINATION DRILL LESSON 31

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Wewe utarudi siku gani?
Nitarudi kesho.

Hao, Juma, watoto, ninyi.

b. Waislamu watapumzika Jumapili?
Watapumzika Ijumaa.

Wamasai, Mswahili, kijana, mama.

c. Mvuvi atavua samaki kesho?
La, atavua samaki Jumamosi.

ninyi, Waswahili, mtoto, wanaume.

d. Ninyi mtahudhuria mashindano yetu?
La, tuna kazi nyingi siku hiyo.

wewe, wakulima, daktari, wenyeji.

e. Mlifanya kazi jana?
Ndio, tulifanya kazi mchana kutwa.

Jumapili, Alhamisi, Ijumaa, Jumamosi.

f. Mtamaliza kazi saa ngapi?
Tutamaliza saa tatu usiku.

anza, fanya, acha.

g. Leo ni siku ya soko?
La, siku ya soko ni Jumatano.

kupumzika, kufanya hazi, kuabudu.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Wiki moja ina siku saba. Kila siku ina jina. Waislamu wanaanza kuhesabu na siku ya Ijumaa. Kwa Waislamu hii ni siku kubwa, ni sikukuu yao. Siku hiyo wanakwenda kuabudu Mungu. Wakristo wanaabudu Mungu siku ya Jumapili.

Siku ya Jumatatu watu wote wanakwenda kazini. Wanaendelea na kazi kila siku hata Jumamosi. Labda wengine watatoka kazini saa sita siku ya Jumamosi.

Hivi tunaona katika kutaja siku tunafuata kalenda ya Waislamu. Wiki yao inaanzia na Ijumaa. Jumamosi ni siku ya kwanza kufuata Ijumaa, Jumapili siku ya pili, Jumatatu siku ya tatu, na hivyo. Siku kabla ya Ijumaa ni Alhamisi. Ali atarudi safarini siku hiyo. Alisafiri siku ya Jumanne.

Step 2. Questions based on the above narration:

Kuna siku ngapi katika juma?
Kila siku ina jina lake?
Ijumaa ni siku kubwa kwa Waislamu?
Wanafanya nini siku hiyo?
Sikukuu ya Wakristo ni siku gani?

Watu wanakwenda kazini siku gani?
Wanaendelea siku za kazi hata lini?
Wakristo wanapumzika siku gani?
Waislamu watafanya kazi Ijumaa?
Wiki ya Waislamu inaanzia siku gani?

Tunafuata kalenda ya Waislamu?
Jumapili ni siku ya ngapi katika kalenda ya Kikristo?
Siku gani inafuata Jumatano?
Ali alikwenda lini safarini?
Na atarudi siku gani?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 32

LESSON 32


JANUARI · MACHI · APRILI · JULAI · AGOSTI · OKTOBA
FEBRUARI · MEI · JUNI · SEPTEMBA · NOVEMBA
DESEMBA
DESEMBA
20

1st PERIOD — PERCEPTION DRILL — LESSON 32

Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drills on dates and months.

a. Mwezi wa Januari.
Mwezi wa Februari.
Mwezi wa Machi.
Mwezi wa Aprili.
Mwezi wa Mei.
Mwezi wa Juni.

b. Mwezi wa Julai.
Mwezi wa Agosti.
Mwezi wa Septemba.
Mwezi wa Oktoba.
Mwezi wa Novemba.
Mwezi wa Desemba.

c. Mwezi huu.
Mwezi ule.
Miezi hii.
Miezi ile.
Mwaka huu.
Mwaka ule.

d. Majira ya joto.
Majira ya baridi.
Majira ya mvua.
Majira ya vuli.
Majira ya masika.
Majira ya Krismasi.

e. Tarehe gani leo?
Leo ni tarehe gani?
Ni tarehe ishirini.
Ni tarehe kumi na mbili.
Utasafiri tarehe gani?
Nitasafiri tarehe kumi.

f. Majina ya Kiingereza.
Majina ya Kizungu.
Majina ya Kiswahili.
Kalenda ya Kizungu.
Kalenda ya Kikristo.
Kalenda ya Kiislamu.

2. Drills relating to time.

a. Saa moja.
Saa moja na robo.
Saa moja kasa robo.
Saa moja na nusu.
Saa moja na dakika tano.

b. Saa moja ina dakika ngapi?
Kuna dakika ngapi katika saa moja?
Katika saa moja kuna dakika sitini.
Katika nusu saa kuna dakika thelasini.
Katika robo saa kuna dakika kumi na tano.

c. Mwezi mmoja una siku ngapi?
Una siku thelasini.
Mwezi una wiki ngapi?
Mwezi una wiki nne.
Mwaka una miezi mingapi?
Mwaka una miezi kumi na miwili.

d. Mwaka una wiki ngapi?
Mwaka una wiki hamsini na mbili.
Wiki moja ina siku ngapi?
Wiki ina siku saba.
Kuna siku ngapi katika juma?
Kuna siku saba katika juma.

e. Sasa ni saa tatu na nusu.
Ni saa tatu asubuhi.
Ni saa tatu usiku.
Ni saa sita sasa.
Saa nne mchana.
Saa nne usiku.

f. Leo asubuhi, saa mbili.
Leo saa sita.
Kesho asubuhi, saa moja.
Kesho jioni, saa kumi na moja.
Jana jioni, saa kumi na nusu.
Jana asubuhi, saa moja na robo.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

2nd PERIOD ENGLISH DIALOGUE LESSON 32

1. How many months are there in a year?

   There are 12 months.

2. Are the months named like in English?

   They are very close to the English.

3. When does it rain there in Tanganyika?

   The big rainy season is in April, May and June.

4. Does it rain only during that season?

   No, it rains a little in the small rainy season.

5. Is the small rainy season in October and November?

   Yes, and the hot months are January and February in particular.

6. The coldest months are in June and July?

   Yes, and in August and September it is very nice.

7. On what date are you travelling?

   I'll travel on the 10th of March.

8. What date is it today?

   Today is the 20th of December.

LESSON 32


1
?
#
JANUARI
JAN 1
12
JANUARI
2
?? =
MARCH
APRIL
JANUARY
JANUARI
MAY
MEI
3
?
?
TANGANYIKA
APRILI
MEI
JUNI
4
5
X,
??
=
OKTOBA
NOVEMBA
JANUARI
FEBRUARI
&
6
??
JUNI
JULAI
AGOSTI
SEPTEMBA
&
7
?
MACHI
10
8
?
=
Desemba
20

1. Katika mwaka kuna miezi mingapi?
Kuna miezi kumi na miwili.

2. Majina ya miezi ni kama ya Kiingereza?
Ni karibu sawa na ya Kiingereza.

3. Kule Tanganyika mvua inanyesha lini?
Majira ya masika ni miezi ya Aprili, Mei, na Juni.

4. Mvua inanyesha katika majira hayo tu?
La, katika vuli kuna mvua kidogo.

5. Majira ya vuli ni Oktoba na Novemba?
Ndio, na miezi ya joto ni Januari na Februari hasa.

6. Miezi ya baridi zaidi ni Juni na Julai?
Ndio, na Agosti na Septemba kuna hali nzuri.

7. Utasafiri tarehe gani?
Nitasafiri tarehe kumi mwezi wa Machi.

8. Leo ni tarehe gani?
Leo ni tarehe ishirini, mwezi wa Desemba.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Tutakaa hapa kwa miezi sita.
Tutakaa hapa kwa miezi sita.

miaka, wiki, siku, saa.

b. Juni ni mwezi wa baridi.
Juni ni mwezi wa baridi.

Septemba, Julai, huu, Desemba.

c. Huo ni mwezi wa mvua.
Huo ni mwezi wa mvua.

Novemba, Agosti, Machi, Mei.

d. Januari na Februari ni miezi ya joto.
Januari na Februari ni miezi ya joto.

mvua, baridi, kazi nyingi.

e. Hali ni nzuri siku hizi.
Hali ni nzuri siku hizi.

miezi, wiki.

f. Nitasafiri tarehe kumi, mwezi wa Mei.
Nitasafiri tarehe kumi, mwezi wa Mei.

rudi, fika, ondoka.

2. Substitution Drill

a. baridi
Mwezi huu kuna ------ nyingi.
Mwezi huu kuna baridi nyingi.

joto, mvua.

b. mitatu.

Alikaa kule miezi ------

Alikaa kule miezi mitatu.

-ingi, -nne, sita, -moja.

c. Tutasafiri

---------- kwa mwezi mmoja.

Tutasafiri kwa mwezi mmoja.

fanya kazi, soma, pigana.

d. Waliongea

--------- kwa saa nyingi.

Waliongea kwa saa nyingi.

safiri, cheza, soma, pumzika.

e. Juni

Mwezi wa ---- kuna mvua.

Mwezi wa Juni kuna mvua.

Julai, Agosti, Septemba, Desemba.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 32

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. Phonological target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the questions and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Huu ni mwezi wa Januari?
2nd: La, ni mwezi wa Desemba.

Agosti, Juni, Februari, Machi.

b. 1st: Tunaingia katika mwezi wa joto?
2nd: La, tunaingia katika mwezi wa mvua.

siku, wiki.

c. 1st: Mtoto huyu ana umri gani?
2nd: Ana umri wa miezi kumi na mmoja.

mnyama, mbwa, ng'ombe, swala.

d. 1st: Kuna miezi mingapi katika mwaka?
2nd: Kuna miezi kumi na miwili.

siku, wiki.

e. 1st: Watarudi mwezi gani?
2nd: Watarudi mwezi wa Mei.

ondoka, shambulia, shindana.

5th PERIOD RECOMBINATION DRILL LESSON 32

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Sisi tutapata mvua mwezi gani?
Tutapata mvua mwezi wa Februari.

ninyi, Watanganyika, kule.

b. Askari watahama lini?
Watahama mwezi wa Aprili.

Hao, wewe, vijana, mvuvi.

c. Utarudi tarehe gani?
Nitarudi tarehe tano mwezi wa Oktoba.

kwenda, pumzika, anza kazi, safiri.

d. Mnapata mvua miezi mingapi kwa mwaka?
Tunapata mvua miezi mitatu.

ruhusa, joto.

e. Utaondoka saa ngapi?
Nitaondoka saa sita kamili.

lala, kula, amka, pumzika.

f. Hii ni saa yako?
La, ni ya Karanja.

mkuki, mikeka, kiti, vitabu.

g. Kijana huyo anapendeza?
Ndio, anapendeza sana.

mti, mishale, vikapu, kikombe.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Katika mwaka kuna miezi kumi na miwili. Kila mwezi una jina, na kwa Kiswahili jina ni karibu sawa na jina la Kiingereza. Katika kalenda Waafrika wanafuata kalenda yetu.

Majira ya Afrika ya Mashariki ni tofauti na majira hapa Amerika. Kule mvua inanyesha zaidi katika miezi ya Aprili, Mei na Juni, ndiyo majira ya masika. Kabla ya masika kuna majira ya joto katika miezi ya Januari na Februari. Lakini miezi ya Juni na Julai kuna baridi sana.

Miezi ya Agosti na Septemba kuna hali nzuri. Hakuna joto kubwa wala baridi. Watu wengi wanakwenda shambani kuvuna wakati huo. Katika miezi ya Oktoba, Novemba, na labda hata Desemba, mvua inaweza kunyesha kidogo. Ni majira ya vuli. Mwezi wa Desemba tuna sikukuu yetu kubwa ya Krismasi.

Step 2. Questions based on the above narration:

Kuna miezi mingapi katika mwaka?
Majina ya miezi ni karibu sawa na ya Kiingereza?
Waafrika wanafuata kalenda yetu?

Kule Afrika majira ni tofauti na hapa?
Tanganyika ni Afrika ya Mashariki?

Majira ya masika ni miezi gani?
Majira ya joto ni baada ya masika?
Hali ya baridi zaidi ni miezi gani?
Majira ya joto ni miezi gani?
Mvua inanyesha zaidi miezi gani?

Tutapata hali nzuri mwezi wa Agosti?
Kuna joto kubwa mwezi wa Septemba?
Watu wanafanya nini shambani miezi hiyo?
Tutapata mvua kidogo mwezi wa Novemba?
Sikukuu kubwa ya Krismasi ni lini?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 33

LESSON 33



1st PERIOD PERCEPTION DRILL LESSON 33

Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on object prefixes.

a. Ni (me)

Aliniona
Aliniambia
Aliniuzia
Aliniuliza
Alinitoza
Alinipa

b. ku (you)

Nilikuambia
Nilikuuliza
Nilikupa
Nilikufuata
Nilikuamini
Nilikudai

c. m (him, her)

Nitamwona
Nitamwambia
Nitamkopesha
Nitampa
Nitamhoji
Nitamwuliza

d. tu (us)

Utatuonyesha
Utatufuata
Utatusaidia
Utatufukuza
Utatuinua
Utatujaribu

e. wa (you) pl. often used with suffix '-ni'

Amewalisha ninyi > amewalisheni
Amewapendeza ninyi > amewapendezeni
Amewaruhusu ninyi > amewaruhusuni
Amewashinda ninyi > amewashindeni
Amewasukuma ninyi > amewasukumeni
Amewatambua ninyi > amewatambueni

f. wa (them)

Tuliwapa
Tuliwatambua
Tuliwataja
Tuliwatunza
Tuliwatayarisha

2. Drill on the relative of time, PO.

a. Niliporudi
Nilipokuja
Niliposafiri
Nilipokwenda
Nilipoamka

b. Alipoandika
Aliposoma
Alipopeleka
Alipocheza
Alipofanya kazi

c. Ulipompa
Ulipomsaidia
Ulipomwona
Ulipomwuliza
Ulipomdai
Ulipomwamini

d. Watakapomhoji
Watakapompiga
Watakapomhukumu
Watakaponiuzia
Watakaponitoza
Watakaponiambia

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

2nd PERIOD ENGLISH DIALOGUE LESSON 33

1. Did Omari cheat you when he sold you the car?
Yes, now I am demanding my money.

2. What did the lawyer ask you when you went to him?
He asked me about the agreement concerning the car.

3. Will he accuse him in court?
He will take the case to court on Tuesday.

4. Did you (pl.) get many witnesses?
Yes, the judge will cross examine them all.

5. Will he decide the case on that day?
I think he will pass judgement on Tuesday.

6. How much will you pay the lawyer?
He charged me fifty pounds (£).

7. Will your brother lend you the money?
No, I shall ask all of you to help me.

8. Do you hope to get justice?
Without a doubt I believe so.

LESSON 33


1
??
Omari
V,
2
?
?
♂
3
??
♂
KORTI
♂
Jumanne
4
??
#
V,
???!
5
??
♂
♂
Jumanne
6
?
$
♂
£50
7
??
X,
8
??

1. Omari alikudanganya alipokuuzia motokaa?
Ndio, sasa ninadai pesa zangu.

2. Wakili alikuuliza nini ulipofika kwake?
Aliniuliza habari za mapatano ya motokaa.

3. Atamshtaki Omari kortini?
Atapeleka kesi kortini Jumanne.

4. Mmepata mashahidi wengi?
Ndio, hakimu atawahoji wote.

5. Ataamua kesi siku hiyo?
Ninadhani atatoa hukumu Jumanne.

6. Utamlipa wakili pesa ngapi?
Alinitoza pauni hamsini.

7. Ndugu yako atakukopesha pesa?
La, nitawaulizeni kunisaidia.

8. Unatumaini kupata haki yako?
Bila shaka ninaamini hivi.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Omari alinidanganya.
Omari alinidanganya.

wewe, wakili, ninyi.

b. Alipofika tulifurahi.
Alipofika tulifurahi.

rudi, ondoka, simama, pumzika.

c. Alimpeleka kortini jana.
Alimpeleka kortini jana.

Jumamosi, juzi, asubuhi.

d. Tutawashtaki wevi.
Tutawashtaki wevi.

mwivi, wewe, ninyi, wageni.

e. Hakimu ataamua kesi kesho.
Hakimu ataamua kesi kesho.

Jumanne, leo, Ijumaa, kesho kutwa.

f. Alitutoza pauni kumi.
Alitutoza pauni kumi.

ishirini, sita, arobaini, nyingi.

2. Substitution Drill

a. mbovu.
Aliniuzia motokaa -----
Aliniuzia motokaa mbovu.

-zee, -zuri, -baya, -pya.

b. pesa
Atanirudishia ---- zangu.
Atanirudishia pesa zangu.

nguo, mikuki, vyombo.

wakili
c. Nilimwamini ------ aliponisaidia.
Nilimwamini wakili aliponisaidia.

daktari (pl.), wewe, walimu.

shahidi
d. Wakili atamhoji ------- kesho.
Wakili atamhoji shahidi kesho.

mwenyeji, ninyi, mimi, wewe.

e. wauzaji
Nitawashtaki ------- hawa.
Nitawashtaki wauzaji hawa.

mkulima, wakili, askari (s.), watu.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 33

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the questions and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Utampeleka kortini?
2nd: Nitampeleka huko kesho.

nyumba, duka, mji, skuli.

b. 1st: Hakimu amewahoji wote?
2nd: Ndio, amewahoji wote.

shahidi, mwanafunzi, wavuvi.

c. 1st: Nani atamshtaki mtu huyo?
2nd: Tutamshtaki wenyewe.

mwivi, watu, mawakili, wakili.

d. 1st: Ulimlipa aliporudi?
2nd: Nilimlipa pauni tano.

faulu, ondoka.

e. 1st: Utatuuliza nini?
2nd: Nitawaulizeni kila kitu.

toza, ambia, dai.

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Omari alikudanganya?
Ndio, alinidanganya.

wevi, mpelelezi, adui (pl.), watoto.

b. Wakili atatuuliza nini?
Atatuuliza habari ile.

mawakili, daktari, ninyi, mkulima.

c. Tutamshtaki Omari?
Tutamshtaki kesho.

vijana, huyo, wavuvi, kijana.

d. Hakimu atawapatieni haki yenu?
Ndio, atatupatia haki yetu.

yao, yako, yetu, yangu.

e. Wakili atawahoji mashahidi?
Ndio, atawahoji Jumanne.

watoto, mwalimu, mkulima, wavuvu.

f. Utamlipa kijana pesa zake?
Atangoja mpaka Jumamosi.

vijana, wakulima, sisi, mimi.

g. Ninyi mtanikopesha pesa?
La, tutamkopesha ndugu yako.

Omari, wewe, mvuvi, walimu.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Siku moja Ali alikwenda kwa Omari kununua motokaa. Omari alisema ana motokaa nzuri sana na alimwuzia Ali motokaa hiyo. Sasa Ali aliendesha motokaa na baada ya siku mbili alianza kupata matata. Alitambua kwamba motokaa ni mzee na mbaya. Aliporudi kwa Omari kudai pesa zake, Omari alisema, "La!"

Sasa Ali alikwenda kwa wakili. Wakili alimwuliza habari ya mapatano juu ya motokaa. Alitambua kwamba Omari amekosa na alisema atamshtaki Omari kortini. Alipeleka kesi kortini Jumanne. Kule hakimu alihoji mashahidi. Halafu aliamua kesi na Ali alipata haki yake. Lakini wakili alimtoza Ali pesa nyingi, pauni hamsini. Ali alikosa pesa hizo na anatafuta rafiki kukopesha pesa. Anaamini atapata bila shaka.

Step 2. Questions based on the above narration:

Nani alimwuzia Ali motokaa?
Omari alisema nini juu ya motokaa hiyo?
Ali alimwamini Omari?
Baada ya kuendesha motokaa siku mbili aliona nini?
Motokaa ilikuwa mpya?

Aliporudi kwa Omari alisema nini?
Ali alikwenda kwa nani halafu?
Wakili alimwuliza nini?
Wakili alisema atamshtaki Omari?
Alipeleka kesi kortini?

Hakimu aliamua kesi hii siku gani?
Hakimu alihoji nani?
Ali alipata haki yake?
Nani alimtoza pauni hamsini?
Nani alikosa pesa?
Atafanya nini kupata pesa?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

ED026651

DEFENSE LANGUAGE INSTITUTE

WEST COAST BRANCH

PRESIDIO OF MONTEREY, CALIFORNIA

РУССКИЙ
СРПСКОХРВАТСКИ
華 語
SHQIP
MAGYAR
日 本 語
TÜRKÇE
PORTUGUÊS
فارسی
ROMÂNĂ
УКРАЇНСЬКА
ITALIANO
BAHASA INDONESIA
ภาษาไทย

SWAHILI

12 WEEKS COURSE

VOLUME IV
LESSONS 34-44

БЪЛГАРСКИ
POLSKI
粵 語
ČESKY
ΕΛΛΗΝΙΚΑ
한 국 어
ESPAÑOL
FRANÇAIS
العربية
SLOVENŠČINA
မြန်မာ ဘာသာ
DEUTSCH
TIẾNG VIỆT NAM
LIETUVIŲ

KISWAHILI

AL 001 753

SWAHILI

12 WEEKS COURSE

Volume IV

Lessons 34-44

March 1963

DEFENSE LANGUAGE INSTITUTE
West Coast Branch
Presidio of Monterey, California

CONTENTS

Page

LESSON 34 503

LESSON 35 517

LESSON 36 531

LESSON 37 545

LESSON 38 559

LESSON 39 573

LESSON 40 587

LESSON 41 601

LESSON 42 615

LESSON 43 629

LESSON 44 643

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 34



Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on the reflexive 'ji'.

a. Amejiumiza.
Amejikata.
Amejichoma.

b. Nimejisaidia.
Nimejifunga.
Nimejipatia.

c. Watajiumiza.
Watajikata.
Watajichoma.

d. Tutajisaidia.
Tutajifunga.
Tutajipatia.

e. Ulijiumiza?
Ulijikata?
Ulijichoma?

f. Mlijisaidia?
Mlijifunga?
Mlijipatia?

g. Kujiumiza.
Kujikata.
Kujichoma.

h. Kujisaidia.
Kujifunga.
Kujipatia.

2. Semantic drills using new lexical items.

a. Ajali mbaya.
Gazeti mbaya.
Dreva mbaya.

b. Kugongana na motokaa.
Kugongwa na motokaa.
Kupinduka na motokaa.

c. Kioo kizuri.
Kipande kizuri.
Kioo kimepasuka.
Kipande kimepotea.

d. Kupinduka.
Kuokoka.
Kuvunjika.
Kupasuka.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. I hear about many accidents.

   True, I read in the papers a child hurt himself.

2. How did he hurt himself? Did he cut himself?

   No, he burnt himself badly by fire.

3. What gives concerning a car which was hit?

   It turned over when it collided with a lorry.

4. Say, did the driver get hurt too?

   Yes, he cut himself when the glass broke.

5. Did the window glass break in pieces (get shattered) ?

   Yes, and passengers cut themselves when they got out.

6. Did they save their lives although they got hurt?

   They got saved, and others helped themselves.

7. How did they help themselves?

   They used 'First Aid'.

8. Did they tie bandages to stop bleeding?

   Yes, and they got medicine for their wounds.

LESSON 34


1
2
?
X,
3
?
4
!
??
V,
5
??
V,
6
??
&
7
?
8
??
V, &

1. Ninasikia habari za ajali nyingi.
   Kweli, nilisoma gazetini mtoto amejiumiza.

2. Amejiumiza kwa njia gani? Amejikata?
   La, amejichoma vibaya kwa moto.

3. Kuna nini juu ya motokaa ilipogongwa?
   Ilipinduka ilipogongana na lori.

4. Je, dreva amejiumiza vilevile?
   Ndio, amejikata kioo kilipovunjika.

5. Kioo cha dirisha kimepasuka vipande?
   Ndio, na abiria walijikata walipotokea.

6. Wameokoka maisha ingawa wameumia?
   Wameokoka, na wengine wamejisaidia.

7. Wamejisaidia kwa njia gani?
   Walitumia "Huduma ya Kwanza."

8. Walijifunga vitambaa kuziba damu?
   Ndio, na walijipatia dawa kwa jeraha.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Ajali mbaya imetokea leo.
Ajali mbaya imetokea leo.

kubwa, -ingi, -ingine, tatu.

b. Tulisoma gazetini watoto wamejiumiza.
Tulisoma gazetini watoto wamejiumiza.

askari, dreva, mvuvi, mkulima.

c. Motokaa zetu zilipinduka zilipogongana.
Motokaa zetu zilipinduka zilipogongana.

-kubwa, -mbili, -dogo, -ao.

d. Ameokoka maisha ingawa amejiumiza vibaya.
Ameokoka maisha ingawa amejiumiza vibaya.

kata, choma.

e. Walijisaidia walipofika.
Walijisaidia walipofika.

funga vitambaa, zoeza, funza, ficha.

d. Dreva amejiumiza vibaya.
Dreva amejiumiza vibaya.

Yusufu, Kapteni, askari (pl.).

2. Substitution Drill

a. yake
Motokaa ---- iligongwa na lori.
Motokaa yake iligongwa na lori.

-etu, -ao, -kubwa, -zee.

b. alimsaidia
Daktari ---------- alipojiumiza.
Daktari alimsaidia alipojiumiza.

-pa dawa, chukua, tunza.

c. Dreva
----- amejiumiza katika ajali.
Dreva amejiumiza katika ajali.

Koplo, mvuvi, wapelelezi, wanaume.

d. Amejisaidia
----------- ingawa amejiumiza vibaya.
Amejisaidia ingawa amejiumiza vibaya.

tunza, funga kitambaa, ficha.

e. walipofika
Walijipatia dawa ---------- nyumbani.
Walijipatia dawa walipofika nyumbani.

ingia, jificha.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning)

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the questions and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Wavuvi walijiumiza wapi?
2nd: Walijiumiza mikono na miguu.

rafiki (s.), daktari (pl.), Wamasai, ninyi.

b. 1st: Ulimfunga kitambaa alipofika?
2nd: Ndio, nilimsaidia sana.

jiumiza, jikata kidole, rudi, jichoma mkono.

c. 1st: Askari alimwonya dreva alipomkamata?
2nd: Ndio, alimwonya.

wakulima, vijana, mwivi.

d. 1st: Wewe ulijisaidia ulipojiumiza?
2nd: Nilijipatia dawa.

Wavuvi, mkulima, wenyeji.

e. 1st: Walinzi wamejisaidia kwa njia gani?
2nd: Walitumia huduma ya kwanza.

mkulima, mvuvi, daktari, wakili.

5th PERIOD RECOMBINATION DRILL LESSON 34

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Wavuvi wamejiumiza vibaya?
Wamejiumiza vibaya sana.

Jemadari, mpelelezi, wanaume, wewe.

b. Mtoto amepata ajali?
Ndio, amejikata kidole.

Hao, mwanamke, kijana, wakulima.

c. Motokaa gani ziligongana?
Motokaa kubwa ziligongana.

-dogo, -pya, -zuri, -zee.

d. Tutajificha wapi?
Tutajificha hapa.

zoeza, funga, saidia.

e. Vioo vilimwumiza Karanja?
Ndio, vilimwumiza zilipopasuka.

wenyeji, wapelelezi, mkulima, wewe.

f. Dreva amejiumiza vilevile?
Amejiumiza kidogo tu.

wanaume, mbwa (pl.), askari.

g. Wewe ulimfunga kitambaa alipojiumiza?
Ndio, nilimfunga kitambaa.

ninyi, Kapteni, wakulima, daktari.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Leo nilisoma katika gazeti habari ya ajali nyingi. Kwanza habari ya mtoto mmoja. Huyo alijiumiza alipoanguka motoni. Alijichoma vibaya katika mikono na miguu. Watu wachache walimsaidia na walimpeleka hospitali.

Halafu nilisoma juu ya ajali ya motokaa. Motokaa iligongana na lori. Ilipogongwa na lori, motokaa ilipinduka. Walikuwa abiria wanne ndani ya motokaa na dreva. Dreva alijiumiza alipojikata kwa kioo. Kioo cha dirisha kilipasuka na vipande vya kioo vilimkata. Abiria walijikata vilevile walipotokea chini ya motokaa. Ingawa waliumia, waliokoka maisha yao. Walifurahi kwa sababu waliokoka. Wamejisaidia upesi walipotumia 'Huduma ya Kwanza'. Walitia dawa kwa jeraha. Halafu walifunga majeraha kwa vitambaa kuziba damu. Baadaye motokaa ya wagonjwa iliwapeleka hospitali vilevile.

Step 2. Questions based on the above narration:

Nilisoma habari gani katika gazeti?
Mtoto alianguka wapi?
Alijiumiza kwa njia gani?

Alijichoma miguu tu?
Watu wachache walimpeleka wapi?

Motokaa iligongwa na nini?
Motokaa ilipinduka ilipogongwa?
Walikuwa abiria wangapi?
Dreva alijiumiza kwa njia gani?
Kioo cha dirisha kilipasuka?

Abiria walitokea wapi?
Walijikata vilevile au walijichoma?
Waliokoka maisha yao?
Wamejisaidia kwa njia gani?
Walitia nini kwa jeraha?
Motokaa ya wagonjwa iliwapeleka wapi?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 35

LESSON 35



Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drills (Imperative with Object)

a.	Ambia!	Mwambie!
	Elekea!	Mwelekee!
	Onyesha!	Mwonyeshe!
	Ita!	Mwite!
b.	(kupa)	Nipe!
	(kupa)	Mpe!
	(kupa)	Wape!
c.	Fuata!	Mfuate!
	Chukua!	Mchukue!
	Piga!	Mpige!
d.	Usifuate!	Usimfuate!
	Usipige!	Usimpige!
	Usiambie!	Usimwambie!

2. Semantic drills.

a. Kaskazini.
Upande wa kaskazini.
Elekea kaskazini.
Afrika ya Kaskazini.

b. Kusini.
Upande wa kusini.
Elekea kusini.
Afrika ya Kusini.

c. Mangharibi.
Upande wa mangharibi.
Elekea mangharibi.
Afrika ya Mangharibi.

d. Mashariki.
Upande wa mashariki.
Elekea mashariki.
Afrika ya Mashariki.

e. Ramani.
Chora ramani.
Fuata ramani.

f. Hatari ya nyoka.
Hatari ya adui.
Hatari ya wanyama.

g. Fyeka kichaka.
Fyeka vichaka.
Fyeka majani.

h. Vuka ng'ambo.
Vuka mto.
Vuka daraja.

Step 3. **Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.**

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Tell the Sgt. we'll cross over today.

   Very well! Will we clear a new path in the forest?

2. Yes, you'll follow the river 2 miles downstream to the ford.

   Shall we take that ford to go across?

3. Yes. Don't take useless baggage, just necessary items.

   We'll take rifles, matchets, a compass and a map.

4. That's it. Explain things clearly to the Sgt.

   We'll need matchets for each person to clear the bush.

5. Don't forget to warn them that there is danger.

   True, danger from the enemy and poisonous snakes.

6. Take some medicine with the 'First Aid' kit.

   Across the river do we proceed North?

7. No, all of you follow the river to the South.

   Then do we enter the forest to the West?

8. No, don't go in that direction, follow the map.

   O.K., I see that you have drawn our path on the map.

LESSON 35


1
2
Maili 2
3
&
4
@
5
6
7
S
W
8

1. Mwambie Sajini tutavuka ng'ambo leo.

   Vema! Tutapasua njia mpya msituni?

2. Ndio, mtafuata mto maili mbili mpaka kivukoni.

   Tutashika kivuko hicho kuvuka ng'ambo?

3. Ndio; msichukue vitu bure, vile vya lazima tu.

   Tutachukua bunduki, panga, dira na ramani?

4. Hasa hivyo. Mpe Sajini maelezo wazi.

   Tutahitaji panga kwa kila mtu kufyeka vichaka.

5. Usisahau kuwaonya kwamba kuna hatari.

   Kweli, hatari za adui na nyoka wenye sumu.

6. Chukueni dawa kwa 'Huduma ya Kwanza'.

   Ng'ambo ya mto tutaendelea kaskazini?

7. La, fuateni mto kuelekea kusini.

   Halafu tutaingia msitu kuelekea magharibi?

8. La, msielekee upande huo, fuateni ramani.

   Vema, ninaona umechora njia yetu katika ramani.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Tutavuka ng'ambo leo.
Tutavuka ng'ambo leo.

ziwa, daraja, mto.

b. Watapasua njia mpya msituni.
Watapasua njia mpya msituni.

-ingi, -ingine, -refu, tatu.

c. Chukueni vitu vya lazima t u.
Chukueni vitu vya lazima tu.

bunduki, risasi, panga, ramani.

d. Mpe Sajini maelezo wazi.
Mpe Sajini maelezo wazi.

Koplo, askari, wakili, daktari.

e. Usisahau kwamba kuna hatari.
Usisahau kwamba kuna hatari.

nyoka, adui, mvua, wapelelezi.

f. Ng'ambo ya mto tutaendelea kaskazini.
Ng'ambo ya mto tutaendelea kaskazini.

kusini, mbele, magharibi, milimani.

2. Substitution Drill

a. ng'ambo.
Tutafaulu kuvuka -------
Tutafaulu kuvuka ng'ambo.

mto, ziwa, daraja.

b. nne.
Walifuata mto maili ---
Walifuata mto maili nne.

moja, mbili, tano, sita.

c. dawa
Chukueni ---- za kutosha.
Chukueni dawa za kutosha.

mikuki, risasi, panga.

d. Ninyi
----- mtaelekea kaskazini.
Ninyi mtaelekea kaskazini.

sisi, wewe, daktari (pl.), wavuvi

e. wavuvi
Fuataneni na ------ ziwani.
Fuataneni na wavuvi ziwani.

wenyeji, Kapteni, Sajini.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 35

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the questions and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Leo tutavuka ng'ambo?
2nd: Tutavuka ng'ambo mara moja.

mto, ziwa, kisiwa, daraja.

b. 1st: Wakulima watapasua njia msituni?
2nd: Ndio, watapasua njia mpya.

wenyeji, ninyi, wanaume, wewe.

c. 1st: Koplo alikupa amri gani?
2nd: Aliniambia nisichukue silaha.

askari, sisi, daktari, wakili.

d. 1st: Karanja alikuambia tulisema nini?
2nd: Aliniambia mlitaka kujificha mjini.

sisi, wapelelezi, vijana, wanaume.

e. 1st: Ninyi mtaelekea upande gani ng'ambo?
2nd: Tutaelekea kusini.

wapelelezi, mwenyeji, mvuvi, wakulima.

5th PERIOD RECOMBINATION DRILL LESSON 35

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Tutavuka ng'ambo siku gani?
Tutavuka ng'ambo Jumanne.

kwenda, rudi, endelea.

b. Wamasai wanajisaidia kwa kufuga wanyama?
Ndio, wanajisaidia sana.

ninyi, Mkikuyu, wewe, wenyeji.

c. Ninyi mtafuata mto mpaka wapi?
Tutafuata mto kwa maili mbili.

wapelelezi, adui, mlinzi, wakulima.

d. Wanafunzi watahitaji panga kufyeka vichaka?
Ndio, watahitaji panga.

mkulima, mwenyeji, wanawake, Mmasai.

e. Uliwaonya wageni kujificha vichakani?
Nilisahau kuwaonya.

mtoto, sisi, Wakikuyu, mvuvi.

f. Mtachukua dawa kwa 'huduma ya kwanza'?
Tutachukua dawa nyingi.

vitambaa, vyombo.

g. Ninyi mtaelekea upande gani kesho?
Kesho tutasafiri kusini.

wanawake, mkulima, adui, mpelelezi.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Kapiteni anamwambia Sajini Meja kwamba watavuka ng'ambo ya mto leo. Halafu wataingia katika msitu mkubwa sana. Msituni hakuna njia. Ni lazima kwa kila askari kuchukua panga. Watatumia panga kufyeka vichaka na kupasua njia mpya msituni.

Kwanza wote watafuata mto maili mbili mpaka kivukoni. Watachukua vitu vya lazima tu kama: bunduki, panga, dira na ramani. Watakapovuka ng'ambo watafuata mto na kuelekea kusini, si kaskazini. Halafu baada ya kwenda maili moja wataingia msituni na kuelekea mashariki. Kapiteni alichora ramani na alionyesha njia mpya katika ramani.

Sajini Meja alionya askari wote juu ya hatari ya adui, na nyoka wenye sumu vilevile. Kama ajali itatukia ni lazima kutumia 'Huduma ya Kwanza'.

Step 2. Questions based on the above narration:

Askari watavuka kwenda wapi?
Wataingia wapi halafu?
Kuna njia gani msituni?

Askari atafanya nini na panga?
Ni lazima kwa kila askari kuchukua panga?

Watafuata mto mpaka wapi?
Watakapovuka ng'ambo watafanya nini?
Watachukua vitu vingi?
Wataelekea kaskazini?
Watahitaji dira na ramani?

Baada ya maili mbili wataingia wapi?
Kapiteni alichora nini?
Watakapoingia msituni wataelekea wapi?
Sajini Meja alionya wote juu ya nini?
Kwa ajali watatumia nini?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 36

LESSON 36



Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on future negative tense.

a. Sitakwenda.
Sitakuja.
Sitakula.
Sitasafiri.

b. Hutangojea.
Hutalala.
Hutalalamika.
Hutanunua.

c. Hatasafiri.
Hatacheza.
Hatauza.
Hatavumilia.

d. Hatutaona.
Hatutaonana.
Hatutapenda.
Hatutafuata.

e. Hamtafyeka.
Hamtaelekea.
Hamtajaribu.
Hamtauliza.

f. Hawatawinda.
Hawatalima.
Hawatavua.
Hawataendesha.

2. Semantic drills.

a. Kwenda pwani.
Kaa pwani.

b. Askari wanalalamika.
Hawatalalamika.

c. Wamekata tamaa.
Hawatakata tamaa.

d. Walionana jana.
Wataonana kesho.

e. Kapteni ana mamlaka.
Huyu hana mamlaka.

f. Kwa gari la moshi.
Safiri kwa gari la moshi.

g. Atangojea stesheni.
Wataonana stesheni.

h. Aliamkia wazazi.
Aliamkia jamaa.

i. Askari watavumilia.
Askari hawatavumilia.

j. Atatungojea.
Hatatungojea.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Why are the soldiers complaining?

   They've given up hope of getting leave today.

2. Will the Captain not come back to see them?

   He won't come back until Monday.

3. Will they not be able to get off even tomorrow?

   They must be a little patient.

4. You yourself have no authority to give leave?

   No, the Captain has that authority.

5. Will you not go to greet your parents?

   I will not be able, because they won't be home.

6. Are you not travelling by car?

   No, I'll travel by train.

7. Will your wife not wait for you at the station?

   She'll wait for me and we'll go to the coast together.

8. Will your children not go along?

   No, they'll stay home with relatives.

LESSON 36


1
2
JUMATAN
3
4
RUHUSA
X,
UHUSA
5
6
X,
7
&
8
X,

1. Mbona askari wanalalamika?
Wamekata tamaa kupata ruhusa leo.

2. Kapteni hatarudi kuonana nao?
Hatarudi mpaka Jumatatu.

3. Hawataweza kupata ruhusa hata kesho?
Ni lazima kuvumilia kidogo.

4. Wewe mwenyewe huna mamlaka kutoa ruhusa?
La, Kapteni ana mamlaka.

5. Hutakwenda kuwaamkia wazazi wako?
Sitaweza, sababu hawatakuwa nyumbani.

6. Hutasafiri kwa motokaa?
La, nitasafiri kwa gari la moshi.

7. Mke wako hatakungojea stesheni?
Ataningojea na tutakwenda pwani pamoja

8. Hamtafuatana na watoto wenu?
La, watabaki nyumbani na jamaa.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Askari wanalalamika.
Askari wanalalamika.

Fatuma, wagonjwa, mgonjwa, wenyeji.

b. Mimi sitalalamika tena.
Mimi sitalalamika tena.

wavuvi, kijana, ninyi, wewe.

c. Sisi hatutakata tamaa mpaka kesho.
Sisi hatutakata tamaa mpaka kesho.

rafiki (pl.), wanaume, mpelelezi, adui (s.).

d. Sitarudi mpaka Jumatatu.
Sitarudi mpaka Jumatatu.

kwenda, jifunza, fanya kazi, pumzika.

e. Hatapata ruhusa leo.
Hatapata ruhusa leo.

toa, uliza, kataa.

f. Hawakuwa na mamlaka hapa.
Hawakuwa na mamlaka hapa.

kazi, wazazi, furaha, nafasi.

2. Substitution Drill

a. wazazi.
Hutakwenda kuwaamkia ------
Hutakwenda kuwaamkia wazazi.

mzazi, ndugu (pl.), rafiki (s.), wazee.

b. Wakulima
-------- hawatakuwa nyumbani.
Wakulima hawatakuwa nyumbani.

mvuvi, sisi, Karanja, daktari (pl.).

c. gari la moshi.
Hatutasafiri kwa ---- -- -----
Hatutasafiri kwa gari la moshi.

motokaa, miguu, ndege, mtumbwi.

d. Rafiki
------ ataningojea stesheni.
Rafiki ataningojea stesheni.

wewe, wakaguzi, mgeni, Waislamu.

e. Sisi
---- hatutafuatana na watoto.
Sisi hatutafuatana na watoto.

Karanja, mvuvi, Wamasai, mimi.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 36

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the questions and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Mbona kijana hatarudi?
2nd: Sababu atakuwa na kazi nyingi.

ninyi, askari, jamaa, wanawake.

b. 1st: Askari watakata tamaa?
2nd: Watavumilia hawatakata tamaa.

mvuvi, wewe, sisi, wauzaji.

c. 1st: Hamtawaamkia wazazi?
2nd: Tutawaamkia kwa furaha.

peleka, uliza, saidia, pokea.

d. 1st: Hawatarudi huko?
2nd: Ndio, hawatarudi huko.

kaa, pumzika, ngoja, endelea.

e. 1st: Hutasafiri Uganda?
2nd: La, sita safiri huko.

Kampala, Nairobi, Mombasa, Entebbe.

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Ali hatacheza mpira?
Hatacheza mpira tena.

wewe, sisi, Kapteni, vijana.

b. Hutapata nafasi kurudi?
Sitapata nafasi.

kusafiri, kutusaidia, kuwafundisha.

c. Hamtawatazama wagonjwa?
Hatutawatazama.

Omari, sisi, Koplo, daktari (pl.).

d. Wenyeji hawatatutisha?
Hawatatutisha.

piga, onyesha, fuata, ona.

e. Hawatawaamkia wazazi wao?
Watawaamkia wazazi wao.

rafiki (s.), wake, mtoto, dada.

f. Wavuvi hawatavua samaki?
Hawatavua samaki leo.

ninyi, vijana, wanaume, wewe.

g. Wewe hutaningojea kando ya mto?
Sitakungojea huko.

hao, mwenyeji, Kapteni, wavuvi, mkulima.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Krismasi ni sikukuu kubwa, na askari walitaka ruhusa kwenda nyumbani. Walimngojea Kapteni muda mrefu. Lakini Kapteni alipeleka habari hatarudi mpaka kesho kutwa. Askari walikata tamaa na walilalamika sana. Sasa hawataweza kwenda nyumbani. Sajini Meja aliwaambia kwamba yeye hataweza kutoa ruhusa, ni lazima kuvumilia. Kapteni tu ana mamlaka kutoa ruhusa.

Baadaye Kapteni alirudi na askari wachache walipata ruhusa. Koplo mmoja alisema hatakwenda nyumbani. Wazazi wake hawatakuwa nyumbani. Sasa atasafiri kwa gari la moshi kwenda pwani. Mke wake atamngojea stesheni na watakwenda pamoja. Lakini watoto hawatakwenda, watakaa nyumbani. Watakaa pamoja na jamaa.

Step 2. Questions based on the above narration:

Kwa nini askari walitaka ruhusa?
Walimngojea nani?
Kapteni atarudi lini?
Askari walifurahi?
Sajini Meja alisema nini?

Nani ana mamlaka kutoa ruhusa?
Askari walivumilia?
Walipata ruhusa baadaye?
Koplo mmoja alipata ruhusa vilevile?
Atakwenda nyumbani?

Wazazi wake watakuwa nyumbani?
Atakwenda wapi sasa?
Atasafiri kwa njia gani?
Mke wake atamngojea wapi?
Watoto watabaki wapi?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 37

LESSON 37



Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on present negative tense.

a. Siendi leo.
Sipendi chai.
Sioni dira.
Sitaki kisu.

b. Hununui kitu.
Hufanyi kitu.
Hutembei leo.
Huangalii watoto.

c. Hali keki.
Hanywi pombe.
Haji kesho.

d. Hatuoni kitu.
Hatuna njaa.
Hatusafiri leo.

e. Hamfanyi kazi.
Hamtengenezi chakula.
Hamfuati amri.

f. Hawasimami vizuri.
Hawafuati ramani.
Hawavui samaki.

2. Semantic drills.

a. Nina njaa.
Sina njaa.

b. Unapenda keki.
Hupendi keki.

c. Ana kiu.
Hana kiu.

d. Tutaburudika kidogo.
Heri kuburudika kidogo.

e. Labda hawezi.
Hawezi kuja.

f. Sukari kwa chai.
Hatutumii sukari.

g. Kutunza afya.
Kuharibu afya.

h. Njaa imezidi.
Watu wamezidi.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

2nd PERIOD ENGLISH DIALOGUE LESSON 37

1. Aren't you going to drink tea today?
   I'm not going, I have no time. Too much work.

2. Never mind, better to refresh (relax) a little.
   O.K., but I can't stay

3. Don't you use milk and a little sugar?
   I don't use sugar, but milk, yes.

4. Don't you like some cake?
   No, I'm not hungry, I'm only thirsty.

5. I don't eat cake, nor does my wife eat it.
   Many people don't use cake much.

6. Why isn't Juma coming these days?
   I don't know, perhaps he can't because he's sick.

7. Doesn't he get medicine.
   I don't think that he lacks medicine.

8. People have got to take care of their health.
   True, health is not to be ruined.

LESSON 37


1
??
2
OK
3
??
&
4
??
X,
5
6
W
Juma
??!
7
??
8

1. Huendi kunywa chai leo?

Siendi, sina nafasi. Kazi imezidi.

2. Si kitu, heri kuburudika kidogo.

Vizuri, lakini siwezi kukaa sana.

3. Hutumii maziwa na sukari kidogo?

Situmii sukari, lakini maziwa, ndio.

4. Hupendi keki kidogo?

La, sina njaa, nina kiu tu.

5. Mimi sili keki, hata mke wangu hali.

Watu wengi hawatumii keki sana.

6. Kwa nini Juma haji siku hizi?

Sijui, labda hawezi sababu ni mgonjwa.

7. Je, hapati dawa?

Sidhani kwamba anakosa dawa.

8. Ni lazima kwa watu kutunza afya.

Kweli, afya si kitu cha kuharibu.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Sinywi kitu leo.
   Sinywi kitu leo.

   taka, tumia, penda, pata.

b. Hutaki kuburudika sasa.
   Hutaki kuburudika sasa.

   enda, acha, anza, hitaji.

c. Hatumii keki.
   Hatumii keki.

   kula, taka, nunua, uza.

d. Hatupati chai hapa.
   Hatupati chai hapa.

   kunywa, chukua, uza, leta.

e. Hamji hapa siku hizi.
   Hamji hapa siku hizi.

   tembea, lima, kaa, lala.

f. Hawaendi Nairobi leo.
   Hawaendi Nairobi leo.

   fika, rudi, kaa, pumzika.

2. Substitution Drill

a. Sitaki
   ------ chakula hiki.
   Sitaki chakula hiki.

   kula, penda, uza, nunua.

1. Huendi kunywa chai leo?
Siendi, sina nafasi. Kazi imezidi.

2. Si kitu, heri kuburudika kidogo.
Vizuri, lakini siwezi kukaa sana.

3. Hutumii maziwa na sukari kidogo?
Situmii sukari, lakini maziwa, ndio.

4. Hupendi keki kidogo?
La, sina njaa, nina kiu tu.

5. Mimi sili keki, hata mke wangu hali.
Watu wengi hawatumii keki sana.

6. Kwa nini Juma haji siku hizi?
Sijui, labda hawezi sababu ni mgonjwa.

7. Je, hapati dawa?
Sidhani kwamba anakosa dawa.

8. Ni lazima kwa watu kutunza afya.
Kweli, afya si kitu cha kuharibu.

b. Huchukui
-------- matunda yale makubwa.
Huchukui matunda yale makubwa.

uza, kula, pata, peleka.

c. Hapendi
------- vitu hivyo.
Hapendi vitu hivyo.

leta, peleka, chukua, tumia.

d. Hatuuzi
------- dawa hapa.
Hatuuzi dawa hapa.

kunywa, pata, nunua, tengeneza.

e. Hamendi
------- huko leo.
Hamendi huko leo.

kaa, lala, tembea, rudi.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 37

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the questions and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Hunywi chai leo?
2nd: Sinywi chai leo.

taka, pata, peleka, uza.

b. 1st: Hapeleki maziwa sokoni?
2nd: Hapeleki maziwa leo.

uza, nunua, pata, ona.

c. 1st: Hatupati maembe mengine?
2nd: Hampati maembe tena.

uza, nunua, peleka, chukua.

d. 1st: Hamli pamoja na watoto?
2nd: Hatuli pamoja.

enda, lima, lala, cheza.

e. 1st: Hawapendi matunda haya?
2nd: Hawapendi matunda hayo.

taka, kula, chukua, uza.

5th PERIOD RECOMBINATION DRILL LESSON 37

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Huchukui mizigo yote?
Sitachukua mizigo yote.

uza, peleka, tumia, nunua.

b. Hauzi viatu vile?
Anasema hatauza viatu vile.

vaa, safisha, chukua, nunua.

c. Hatuli matunda mengine?
Hamtakula mengine.

uza, nunua, pata, peleka.

d. Hamendi Nairobi leo?
Hatutakwenda Nairobi.

rudi, safiri, fika, lala.

e. Hawapeleki barua hizi?
Hawatapeleka barua hizo.

soma, weka, maliza, funga.

f. Sipati maziwa mazuri?
Hutapata maziwa.

kunywa, peleka, chukua, uza.

g. Huuzi shamba lile.
Sitauza shamba hilo.

nunua, lima, pata, taka.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Maofisa wawili walikutana njiani. Mmoja anakwenda mgahawani na mwingine ofisini. Yule wa kwanza anasema: "Njoo mgahawani kwa chai kuburudika kidogo". Lakini mwingine anasema hawezi, hana nafasi, kazi imezidi. Yule wa kwanza anasema "Si kitu, ni vizuri kutunza afya na kuburudika". Sasa yule mwingine alikubali na alikwenda pamoja.

Kule mgahawani waliketi karibu na meza na walijipatia chai. Mmoja anatumia maziwa, mwingine hatumii sukari. Mmoja anakula keki, mwingine hali keki, anasema hana njaa, ana kiu tu.

Rafiki yao, Juma, ni mgonjwa. Hawezi kufika mgahawani. Walitambua ya kwamba afya ni kitu cha kutunza sana. Ugonjwa unaleta hasara, si faida.

Step 2. Questions based on the above narration:

Nani alikutana njiani?
Wa kwanza alikwenda wapi?
Wa pili alikwenda wapi?
Wa pili alikuwa na nafasi?
Kwa sababu alikosa nafasi?

Yule wa kwanza alisema nini?
Wa pili alikubali kwenda pamoja?
Wote walitumia maziwa na sukari?
Wote walikula keki?
Kuburudika ni njia ya kutunza afya?

Nani mgonjwa?
Anaweza kufika mgahawani?
Walitambua nini?
Ugonjwa unaleta faida?
Juma ni rafiki yao?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 38

LESSON 38



Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on Ma class words.

a.

Shamba hili.	Mashamba haya.
Tunda hili.	Matunda haya.
Embe hili.	Maembe haya.
Chungwa hili.	Machungwa haya.

b.

Soko lile.	Masoko yale.
Nanasi lile.	Mananasi yale.
Daraja lile.	Madaraja yale.
Dirisha lile.	Madirisha yale.

c.

Jina fupi.	Majina mafupi.
Ua zuri.	Maua mazuri.
Gari dogo.	Magari madogo.
Jeraha kubwa.	Majeraha makubwa.

d. Majani marefu.
Mavuno mengi.
Mahindi machache.
Maziwa matamu.

e. Mazoezi mengine.
Matata mabaya.
Majira mafupi.
Maisha marefu.

f.

Shamba langu.	Mashamba yangu.
Tunda langu.	Matunda yangu.
Embe langu.	Maembe yangu.
Chungwa langu.	Machungwa yangu.

g.

Soko lako.	Masoko yako.
Nanasi lako.	Mananasi yako.
Daraja lako.	Madaraja yako.
Dirisha lako.	Madirisha yako.

h.

Jina lake.	Majina yake.
Ua lake.	Maua yake.
Gari lake.	Magari yake.
Jeraha lake.	Majeraha yake.

i. Majani yetu.
Mavuno yetu.
Mahindi yetu.
Maziwa yetu.

j. Mazoezi yenu.
Matata yenu.
Majira yenu.
Maisha yenu.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Do all these gardens belong to natives?
   Yes, they grow various crops.

2. Do they grow fruit as well?
   They grow many kinds of fruit.

3. Do pineapples grow well here?
   Look yonder, people are harvesting pineapples.

4. Did you get to taste their oranges?
   Yes, they are very sweet.

5. Say, do they grow mangoes too?
   Yes, there are many fields with mangoes.

6. Is this a corn field?
   That's a field for corn and beans.

7. Where do they sell their crops?
   They have small markets in the villages.

8. Do they sell fruit in the big cities?
   Yes, even in distant lands.

LESSON 38


1
2
3
4
5
Miembe
6
&
7
SOKO
8

2nd PERIOD

SWAHILI DIALOGUE

1. Mashamba haya yote ni ya wenyeji?
Ndio, wanapanda mimea mbalimbali.

2. Wanapanda matunda pia?
Wanapanda matunda ya aina nyingi.

3. Mananasi yanaota vizuri hapa?
Angalia kule, watu wanavuna mananasi.

4. Umepata kuonja machungwa yao?
Ndio, ni matamu kweli.

5. Je, wanapanda maembe vilevile?
Ndio, kuna mashamba mengi ya maembe.

6. Shamba hili ni la mahindi?
Hilo ni la mahindi na maharagwe.

7. Mavuno yao wanauza wapi?
Wana masoko madogo katika kijiji.

8. Wanauza matunda katika miji mikubwa?
Ndio, hata katika nchi za mbali.

PATTERN DRILL I

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Mimi nina shamba.
Mimi nina shamba.

embe, nanasi, ua, tunda.

b. Wanataka kuvuna mahindi.
Wanataka kuvuna mahindi.

matunda, maua, machungwa, mananasi.

c. Tajiri aliwapa shamba hili.
Tajiri aliwapa shamba hili.

tunda, chungwa, nanasi, ua.

d. Ninauza matunda haya.
Ninauza matunda haya.

mashamba, maua, maembe, mananasi.

e. Ninataka kununua tunda lile.
Ninataka kununua tunda lile.

ua, chungwa, embe, nanasi.

f. Atapeleka mananasi yale sokoni.
Atapeleka mananasi yale sokoni.

matunda, maua, machungwa, mahindi.

2. Substitution Drill

a. ua.
Anataka kupanda --
Anataka kupanda ua.

matunda, mchungwa, mwembe, minanasi.

b. ua
Tulinunua -- zuri.
Tulinunua ua zuri.

embe, tunda, chungwa, nanasi.

c. mananasi
Walivuna -------- makubwa.
Walivuna mananasi makubwa.

maua, maembe, matunda, machungwa.

d. Tunda
----- hilo linapendeza.
Tunda hilo linapendeza.

ua, nanasi, embe, chungwa.

e. mashamba
Watauza -------- haya madogo.
Watauza mashamba haya madogo.

matunda, mananasi, maua, maembe.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning)

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the questions and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Wanauza mananasi matamu?
2nd: Ndio, wanauza mananasi matamu.

matunda, maembe, machungwa.

b. 1st: Tutaleta embe hili kubwa?
2nd: La, leteni lile dogo.

tunda, nanasi, embe, chungwa.

c. 1st: Maembe hayo hayatoshi?
2nd: Hayo hayatoshi kabisa.

mashamba, mahindi, maharagwe, mananasi.

d. 1st: Tunda hilo ni tamu?
2nd: Ni tamu kama sukari.

nanasi, chungwa, embe.

e. 1st: Watauza wapi maembe haya?
2nd: Watauza maembe haya sokoni.

matunda, maharagwe, maua, mananasi.

5th PERIOD

RECOMBINATION DRILL

LESSON 38

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Mnataka maziwa mazuri?
   Tunataka maziwa mengi mazuri.

   matunda, maji, maharagwe, mahindi.

b. Alinunua tunda kubwa?
   Alinunua tunda dogo tu.

   nanasi, shamba, embe, chungwa.

c. Maembe haya wametoka wapi?
   Maadui hawa wametoka mbali.

   maharagwe, maji, maua, matunda.

d. Atatumia jina hili kule?
   Ndio, atatumia jina hili.

   tunda, nanasi, embe, chungwa.

e. Ulinunua wapi maua yale?
   Nilinunua maua yale sokoni.

   mahindi, maziwa, matunda, maembe.

f. Unauza embe lile?
   Embe lile siuzi.

   shamba, ua, nanasi, chungwa.

g. Utapeleka maua hayo?
   Sitapeleka maua hayo.

   maharagwe, matunda, mananasi, maembe.

6th PERIOD SITUATIONAL APPLICATION LESSON 38

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Wenyeji wengi wamepanda mimea mbalimbali katika mashamba yao. Walipanda wakati wa mvua na mimea ilotokea na kuota vizuri. Sasa wanajitayarisha kwa mavuno.

Katika shamba moja kuna mahindi na maharagwe. Wengine wanatunza matunda vilevile na kuna miti ya matunda, hasa michungwa na miembe. Kutoka miti hiyo wanavuna machungwa na maembe. Wenyeji wengine wamepanda nanasi na sasa wanavuna mananasi matamu.

Wenyeji wanakaa katika kijiji kidogo hapa karibu na wanapeleka mavuno sokoni kwa lori. Kule sokoni wanunuzi watapeleka matunda yale makubwa na mazuri katika soko kubwa la Nairobi. Labda mengine watayapeleka katika nchi ya mbali.

Step 2. Questions based on the above narration:

Nani amepanda mimea?
Walipanda mimea ya namna gani?
Walipanda wakati gani?
Mimea iliota vizuri?
Wanajitayarisha kufanya nini?

Walipanda mahindi pamoja na nini?
Kutoka michungwa watavuna nini?
Kutoka miembe watavuna nini?
Walipanda matunda gani tena?
Hayo yalikuwa matamu?

Wenyeji wanakaa wapi?
Wanapeleka wapi mavuno?
Watayapeleka kwa njia gani?
Wanunuzi watapeleka wapi matunda?
Unafikiri mengine yatakwenda mbali?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 39

LESSON 39



PERCEPTION DRILL

Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on the past negative tense.

a. Hakuweza.
Hakuenda.
Hakufanya.
Hakutaka.

b. Hawakufuga.
Hawakupika.
Hawakuona.
Hawakufuatana.

c. Sikutembelea.
Sikufurahi.
Sikupata.
Sikuonyesha.

d. Hatukupenda.
Hatukuja.
Hatukula.
Hatukunywa.

e. Hukumaliza.
Hukurudi.
Hukuandika.
Hukutembelea.

f. Hamkufuatana.
Hamkukutana.
Hamkushambulia.
Hamkupigana.

2. Semantic drills.

a. Anafuga kuku.
Mayai ya kuku.
Yai la kuku.

b. Walipungua mia.
Hawakupungua mia.
Mavuno yalipungua.

c. Alitutembelea.
Alimtembelea.
Anatembelea jirani.

d. Bibi anapika chakula.
Mama anapika wali.
Alitupikia nyama.

e. Tulikutana njiani.
Walikutana mjini.
Hawakukutana leo.

f. Bwana Kagema.
Bwana na Bibi.
Bibi Kagema.

g. Mia mbili.
Hawakupungua mia.
Mia na kumi.

h. Yeye ni mzuri mno.
Yeye ni mzuri sana.
Yeye ni mzuri kabisa.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Did you not visit old man Salimu yesterday?
Yes, I went to visit Kagama.

2. Did your friends not go along?
We did not go together, we met at Kagemas.

3. Didn't Mr. & Mrs. Kagema welcome you well?
They welcomed us very well indeed.

4. Weren't you glad to see the many things there?
We were glad to see many things.

5. Did Kagema show you his cattle?
He didn't show us cattle, only the chickens.

6. About how many chickens were there?
There were no less than 200.

7. Did you see the eggs these chickens laid?
We did not see many eggs.

8. Did Mrs. Kagema cook some eggs for you?
She cooked meat and rice for us.

LESSON 39


1
SALIMU
Kagema
2
Kagema's
3
Bw. & Bi. K.
4
5
K
6
200
7
8
Bi. K

1. Hukumtembelea mzee Salimu jana?
   Ndio, nilikwenda kumtembelea Kagema.

2. Hukufuatana na rafiki yako?
   Hatukuenda pamoja, tulikutana kwa Kagema.

3. Bwana na Bibi Kagema hawakukaribisha ninyi?
   Walitukaribisha vema sana.

4. Hamkufurahi kuona vitu vingi huko?
   Tulifurahi kuona mambo mengi.

5. Kagema aliwaonyesheni ng'ombe zake?
   Hakutuonyesha ng'ombe, alituonyesha kuku tu.

6. Kuku hawa walikuwa wangapi?
   Hawakupungua mia mbili.

7. Mliona mayai ya kuku hawa?
   Hatukuona mayai mengi mno.

8. Bibi Kagema aliwapikieni mayai?
   Alitupikia nyama na mchele.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Sikumtembelea jana.
Sikumtembelea jana.

ona, piga, onyesha, pendeza.

b. Hukuwapikia kitu.
Hukuwapikia kitu.

onyesha, kupa, uliza.

c. Hakupeleka mayai.
Hakupeleka mayai.

pika, uza, kula, nunua.

d. Hatukuona kuku.
Hatukuona kuku,

kula, uza, chukua, pata.

e. Hamkuuliza maswali.
Hamkuuliza maswali.

jibu, andika, soma, ona.

f. Hawakuchukua mikeka.
Hawakuchukua mikeka.

safisha, uza, nunua, pata.

2. Substitution Drill

a. Sikupenda
--------- nyama.
Sikupenda nyama.

kula, pata, maliza, choma.

b. Hukuandika
---------- barua.
Hukuandika barua.

pata, ngojea, fungua, tazama.

c. Hakubomoa
--------- nyumba.
Hakubomoa nyumba.

fagia, safisha, chungua, ona.

d. Hatukulima
---------- shamba.
Hatukulima shamba.

pima, taja, tambua, angalia.

e. Hamkupanga
---------- mizigo.
Hamkupanga mizigo.

rudisha, poteza, ngojea, inua.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning)

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the questions and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Hukumtembelea Salimu?
2nd: Nilimtembelea jana.

ona, fukuza, ngojea, shika.

b. 1st: Hakutayarisha mayai?
2nd: Alitayarisha yote.

kula, pima, tumia, angalia.

c. 1st: Hatukufunga mlango?
2nd: Tulifunga mlango.

bomoa, tayarisha, pasua, inua.

d. 1st: Hamkufukuza wevi?
2nd: Tulifukuza wevi wote.

kamata, ona, shambulia.

e. 1st: Hawakupeleka mizigo?
2nd: Walipeleka mizigo juzi.

chukua, panga, tafuta, tayarisha.

RECOMBINATION DRILL

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Huoni ufunguo?
Ninaona ufunguo sasa.

taka, tafuta, peleka, chukua.

b. Hataondoka jioni?
Ataondoka kesho.

lima, fanya kazi, fika, pika.

c. Hamkupata pesa?
Tulipata pesa nyingi.

rudisha, weka, pokea, lipa.

d. Hawakununua mayai?
Walinunua mayai mengi.

kula, uza, peleka, pata.

e. Hatutafaulu leo?
Tutafaulu bila shaka.

kwenda, ondoka, tafuta, pumzika.

f. Hukutafuta mbuzi?
Nilitafuta mbuzi jana.

iba, poteza, nunua, peleka.

g. Hamtaingia nyumbani?
Tutaingia jioni.

kwenda, rudi, lala, ngoja.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Mzee Salimu anaishi katika kijiji. Nilifikiri Juma alikwenda kumwamkia. Lakini yeye hakuenda kumtembelea Salimu jana, alikwenda kwa Kagema.

Kagema ni mtu tajiri. Anafuga ng'ombe wazuri sana na anapata maziwa tele. Anapeleka maziwa sokoni halafu. Vilevile ana kuku wengi wakubwa. Mayai ya kuku hawa ni makubwa.

Juma alifika kwa Kagema pamoja na rafiki zake. Kagema aliwakaribisha vema sana. Bi. Kagema alitengeneza chakula kizuri. Aliwapikia nyama ya kuku na mchele. Bw. Kagema aliwaonyesha wageni wake mambo mengi, hasa kuku, Anafuga kuku wengi, labda kama mia tatu hivi. Juma alifurahi kuona yote. Labda atajaribu kufuga kuku vilevile.

Step 2. Questions based on the above narration:

Nani anaishi katika kijiji?
Juma alikwenda kumwamkia?
Alimtembelea nani basi?
Alikwenda leo au jana?
Kagema ni mtu maskini?

Kagema anafuga nini?
Anapata nini kutoko ng'ombe zake?
Anapeleka nini sokoni?
Anafuga kuku vilevile?
Mayai ni madogo na mabaya?

Kagema alikaribisha wageni vizuri?
Bi. Kagema alitengeneza nini?
Bw. Kagema aliwaonyesha nini?
Anafuga kuku mia ngapi?
Unafikiri Juma atafuga kuku vilevile?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 40


SAFARI
KENYA
TIKITI

1st PERIOD

PERCEPTION DRILL

LESSON 40

Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on the JA negative tense.

a. Sijafunga.
Sijafika.
Sijanunua.
Sijaona.

b. Hatujafunga.
Hatujafika.
Hatujanunua.
Hatujaona.

c. Hujajua.
Hujaona.
Hujatembelea.
Hujasoma.

d. Hamjajua.
Hamjaona.
Hamjatembelea.
Hamjasoma.

e. Hajaja.
Hajala.
Hajanywa.
Hajampa.

f. Hawajaja.
Hawajala.
Hawajanywa.
Hawajampa.

2. Semantic drills.

a. Hajanunua tikiti.
Amepata tikiti.
Bei ya tikiti.
Gharama ya tikiti.

b. Ruka kwa ndege.
Ruka kama ndege.
Ruka juu.
Ruka handaki.

c. Nyati ni mnyama.
Tembo ni mnyama.
Twiga ni mnyama.
Simba ni mnyama.

d. Nina nafasi.
Sina nafasi.
Ninakosa nafasi.
Sijapata nafasi.

e. Safiri kwa ndege.
Safiri kwa meli.
Safiri kwa motokaa.

f. Wakati ujao.
Mwezi ujao.
Mwaka ujao.

g. Alikata neno.
Alikata shauri.
Alikata kwa kisu.

h. Alikwisha kuona.
Alikwisha kwenda.
Alikwisha safiri.

i. Gazeti la Kiswahili.
Gazeti la Kiingereza.
Gazeti lenye picha.

j. Kupiga picha.
Kupiga ripoti.
Kupiga kelele.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

ENGLISH DIALOGUE

1. Did you get ready to travel to Kenya?

   We have not packed all things yet.

2. Are you expecting to fly?

   We have not decided yet, nor have I bought a ticket yet.

3. Did you ask the cost of a ticket to Nairobi?

   I have not asked yet, I'll go and ask tomorrow.

4. Have you read up on animals there?

   Not yet, can you tell us a little?

5. This magazine shows pictures of animals there.

   Look, here's a buffalo and an elephant.

6. I have not seen a buffalo yet, but I've seen a lion.

   Did you visit East Africa yourself?

7. I have not been there yet, I hope to go next year.

   Do you know that our children are coming along?

8. I'm sure that they have not had a chance like this.

   We are all hoping to get there.

LESSON 40


1
??
KENIA
2
??
Tikiti
£
3
??
NAIROBI
4
??
??
5
!
6
??
AFRIKA YA MASHARIKI
7
??
8
!

2nd PERIOD SWAHILI DIALOGUE LESSON 40

1. Umejitayarisha kusafiri Kenya?
Bado hatujafunga mizigo yote.

2. Mnatumaini kuruka kwa ndege?
Hatujakata neno, wala sijanunua tikiti.

3. Umeuliza bei ya tikiti mpaka Nairobi?
Sijauliza, nitakwenda kuuliza kesho.

4. Mmesoma habari za wanyama wa huko?
Hatujasoma, Unaweza kutueleza kidogo?

5. Gazeti hili linaonyesha picha za wanyama wa huko.
Lo! Hapa ni nyati na tembo.

6. Mimi sijaona nyati lakini nimeona simba.
Umetembelea Afrika Mashariki mwenyewe?

7. Sijafika huko, ninatumaini kwenda mwaka ujao.
Unajua watoto wangu watafuatana na sisi?

8. Nina hakika hawajapata nafasi kama hii.
Sote tunatamani sana kufika kule.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Sijafunga mizigo.
Sijafunga mizigo.

leta, pokea, rudisha, peleka.

b. Hujaona nyati.
Hujaona nyati.

kamata, winda, ua, tazama.

c. Hajatamani kuwinda nyati.
Hajatamani kuwinda nyati.

rudi, safiri, endelea, taka.

d. Hatujafagia nyumba.
Hatujafagia nyumba.

nunua, bomoa, ona, tafuta.

e. Hamjasafiri Kenya.
Hamjasafiri Kenya.

rudi, ishi, fika, ondoka.

f. Hawajasoma vitabu.
Hawajasoma vitabu.

nunua, tafuta, pata, panga.

2. Substitution Drill

a. Sijamwona
--------- kijana huyo.
Sijamwona kijana huyo.

uliza, fundisha, tuma, ambia.

b. Hujanieleza
----------- kazi.
Hujanieleza kazi.

fundisha, onyesha, andika.

c. Hajanunua
--------- viatu.
Hajanunua viatu.

safisha, ona, peleka, uza.

d. Hawajakuona.

Hawajakuona.

uliza, tuma, onya, fundisha.

e. Hamjatupa
--------- chakula.
Hamjatupa chakula.

tafuta, pika; uza, peleka.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning)

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the questions and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Mke wako amefunga mizigo?
2nd: Hajafunga mizigo.

nunua, peleka, uza, leta.

b. 1st: Umeona wanyama hao?
2nd: Sijaona wanyama hao.

ua, winda, fukuza, tazama.

c. 1st: Mmenunua tikiti?
2nd: Hatujanunua tikiti.

uza, pata, onyesha, andika.

d. 1st: Wamekueleza habari yote?
2nd: Hawajanieleza bado.

uliza, fundisha, ambia.

e. 1st: Umesoma gazeti leo?
2nd: Sijasoma gazeti.

ona, nunua, uza, pata.

5th PERIOD

RECOMBINATION DRILL

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Ametuambia nini?
Hajatuambia kitu.

kupa, eleza, uliza, onyesha.

b. Umeona nyati?
Sijaona nyati.

ua, winda, tazama.

c. Mmemaliza kusoma?
Hatujamaliza kusoma.

anza, kata neno, jifunza, jua.

d. Hawakukusaidia jana?
La, hawakunisaidia.

piga, fundisha, ona, tafuta.

e. Hamjakunywa dawa?
Hatujakunywa dawa.

pata, leta, nunua, peleka.

f. Wamesafisha nyumba?
Hawajasafisha nyumba.

fagia, nunua, uza, bomoa.

g. Hajapata chakula?
Hajapata chakula.

pika, kula, leta, kosa.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Bw. na Bi. Brauni wanajitayarisha kusafiri Kenya. Bado hawajafika kule. Wanajua kwamba ni mbali na gharama ni kubwa. Hivyo baba hajakata neno kama watasafiri kwa ndege au kwa meli. Sijui, lakini ninafikiri wataruka kwa ndege sababu hawana nafasi kukaa siku nyingi.

Bw. Brauni hajanunua tikiti, lakini atanunua kesho. Sasa alitaka kusikia habari ya wanyama. Nilileta gazeti na picha kumwonyesha. Katika gazeti hilo tuliona picha ya nyati, tembo, simba, twiga na wanyama wengine. Bw. Brauni alitaka kupiga picha ya wanyama na alijitayarisha kufanya hivyo. Watoto na Bi. Brauni wanataka kuona wanyama hawa vilevile na wanafurahi kupata nafasi kama hii. Wao hawajafika Afrika bado.

Step 2. Questions based on the above narration:

Nani anajitayarisha kusafiri Kenya?
Walifika Afrika safari nyingine?
Gharama ya safari itakuwaje?
Baba alikata neno ya safari kabisa?
Wataruka kwa ndege?

Kwa nini watasafiri kwa ndege?
Bw. Brauni amekwisha nunua tikiti?
Atanunua lini tikiti?
Alitaka kusikia habari gani sasa?
Kuna nini katika gazeti?

Waliona picha za wanyama gani?
Bw. Brauni alitaka kuwinda?
Alijitayarisha kufanya nini hasa?
Watoto na Bi. Brauni walitaka nini?
Wamekwisha fika Afrika safari nyingine?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 41

LESSON 41



1st PERIOD ## PERCEPTION DRILL **LESSON 41**

Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on negative tenses - generalization.

a. Anapenda.
Anampa.
Anakula.
Anakunywa.

b. Hapendi.
Hampi.
Hali.
Hanywi.

c. Tutakuja.
Tutachukua.
Tutashambulia.
Tutashinda.

d. Hatutakuja.
Hatutachukua.
Hatutashambulia.
Hatutashinda.

e. Nilipata.
Niliweza.
Nilijua.
Nilijifunga.

f. Sikupata.
Sikuweza.
Sikujua.
Sikujifunga.

g. Wamemwambia.
Wamempa.
Wamemwona.
Wamemrukia.

h. Hawajamwambia.
Hawajampa.
Hawajamwona.
Hawajamrukia.

2. Semantic drills.

a. Alilala chini.
Alilala kitandani.
Alilala kifudifudi.

b. Upepo baridi.
Upepo unavuma.
Upepo mkali.

c. Anavaa kofia.
Kofia ya kawaida.
Kofia ya chuma.

d. Waliogopa mtego.
Waliogopa adui.
Waliogopa wanyama.

e. Walisimamisha adui.
Walirukia adui.
Walipigana na adui.

f. Mabeti ya askari.
Mabeti mengi.
Mabeti begani.

g. Jicho jeusi.
Jicho kubwa.
Jicho langu.

h. Macho meusi.
Macho makubwa.
Macho yangu.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

2nd PERIOD ENGLISH DIALOGUE LESSON 41

1. Is it midnight now?

Yes, a cold wind blows from the mountain.

2. Are you going to the concealment to spy on the enemy?

We'll leave soon and we'll hide ourselves by the road.

3. Will you wear green colored garments?

Yes, we'll also wear steel helmets.

4. Are you taking pistols and machine guns?

Yes, and we'll strap the equipment on our shoulders.

5. You'll wait quietly there by the road?

Yes, we'll lie face downward in the grass and watch.

6. Will the enemy come in a motor vehicle?

Yes, we'll put a large log across the highway.

7. Will the enemy not suspect a trap and retreat?

We'll get a chance to leap on them and overpower them.

8. Don't you think that they will overpower you?

Our soldiers are brave and they know their job.

LESSON 41


1
??
V,
2
??
3
??
V,
4
??
&
V, &
5
??
V,
6
??
ADUI
V,
7
??
8
??
&

1. Sasa ni saa sita usiku?

   Ndio, upepo wa baridi unavuma kutoka milimani.

2. Mtakwenda mafichoni kuvizia adui?

   Tutaondoka karibuni na tutajificha kando ya njia.

3. Mtavaa nguo za rangi ya majani?

   Ndio, tutavaa hata kofia za chuma.

4. Mtachukua bastola na bunduki za bombomu?

   Ndio, na tutajifunga mabeti mabegani.

5. Mtangoja kimya pale njiani?

   Ndio, tutalala kifudifudi nyasini na tutakuwa macho.

6. Adui watakuja kwa motokaa?

   Ndio, tutaweka gogo kubwa kukingama barabara.

7. Adui hawataona mtego na kurudi nyuma?

   Hapo tutapata nafasi kuwarukia na kuwashinda.

8. Hufikiri wataweza kuwashinda ninyi?

   Askari wetu ni hodari na wanajua kazi yao.

PATTERN DRILL I

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Nitavizia adui usiku huu.
Nitavizia adui usiku huu.

ngojea, shambulia, rukia, chungua.

b. Hutaona vijana hao.
Hutaona vijana hao.

tafuta, shinda, fukuza, penda.

c. Aliondoka kuvizia adui.
Aliondoka kuvizia adui.

penda, furahi, kataa, rudi.

d. Hatukulala usiku mzima.
Hatukulala usiku mzima.

jifunza, cheza, soma, kula.

e. Mnachukua bastola.
Mnachukua bastola.

safisha, peleka, tumia, taka.

f. Hawatangoja barabarani.
Hawatangoja barabarani.

kwenda, simama, tembea, cheza.

2. Substitution Drill

a. Hatavizia
--------- adui jioni.
Hatavizia adui jioni.

fukuza, chungua, tafuta, shambulia.

b. Utalala
------- mjini.
Utalala mjini.

rudi, kaa, kwenda, ngoja.

c. Waliumia
-------- macho.
Waliumia macho.

funga, kuwa, fungua, safisha.

d. Hamtabeba
--------- mabeti mabegani.
Hamtabeba mabeti mabegani.

chukua, jifunga, hitaji, weka.

e. Hawakuweka
---------- gogo barabarani.
Hawakuweka gogo barabarani.

peleka, tia, ona, rudisha.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning)

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the question and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Anaumia macho?
2nd: Ndio, anaumia macho.

fungua, funga, safisha, kuwa.

b. 1st: Hamkuvizia adui?
2nd: Hatukuvizia adui.

fukuza, ona, ua, kamata.

c. 1st: Hutapata bastola?
2nd: Sitapata bastola.

chukua, tumia, nunua, hitaji.

d. 1st: Mmevaa kofia za chuma?
2nd: Hatujavaa kofia za chuma.

tafuta, tumia, pata, rudisha.

e. 1st: Unafikiri kwenda nyumbani?
2nd: Sifikiri kwenda huko.

taka, tamani, ngojea, jitayarisha.

RECOMBINATION DRILL

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Hamchukui bunduki za bomubomu?
Hatuchukui bunduki.

tumia, taka, leta, pata.

b. Walivizia adui jana?
Hawakuvizia adui.

fuata, shambulia, chungua, tafuta.

c. Ataona mtego huu?
Hataona mtego huu.

fyatua, haribu, tazama, tengeneza.

d. Umevaa kofia mpya?
Sijavaa kofia mpya.

pata, chukua, nunua, rudisha.

e. Hawakuwa macho?
Walikuwa macho.

safisha, umia, funga, fungua.

f. Hatalala nyasini?
Hatalala nyasini.

kaa, simama, jificha, ngoja.

g. Mlitumia bastola?
Hatukutumia bastola.

nunua, iba, pata, leta.

SITUATIONAL APPLICATION

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Kikosi kidogo cha askari zetu kilitokea usiku kabisa - saa sita usiku. Walivaa nguo rangi ya majani na kofia za chuma. Walivaa mabeti mabegani na kwa silaha walichukua bastola na bunduki ya bombomu. Hivi walikwenda kimya kwa maficho yao kando ya barabara.

Kabla ya kujificha walitia gogo kubwa la mti kukingama barabara. Hivi walikusudia kusimamisha motokaa za adui.

Walipolala kimya kifudifudi katika nyasi walisikia motokaa inakuja. Walijitayarisha kurukia adui. Walijua kwamba adui atasimama na kufikiri watafanyaje. Basi adui walipofika waliwarukia ghafla na baada ya kupigana kifupi waliwashinda na kuwafunga.

Step 2. Questions based on the above narration:

Kikosi kiliondoka saa ngapi?
Askari walivaa nini?
Walifunga nini mabegani?
Walichukua silaha gani?
Walikwenda wapi?

Maficho yalikuwa wapi?
Walitia nini barabarani?
Walikingama barabara?
Walikusudia kufanya nini?
Walifanya kelele?

Walilala kwa njia gani?
Walilala wapi?
Walisikia nini?
Walifanya nini kwa adui?
Waliwashinda?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 42

LESSON 42

PERCEPTION DRILL

1st PERIOD

Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on indirect commands.

a. Lazima afanye.
Lazima aende.
Lazima wawe tayari.
Lazima wajiweke tayari.

b. Mwambie aende.
Mwambie afanye.
Mwambie atengeneze.
Mwambie ajifiche.

c. Waamrishe watayarishe ndege.
Waamrishe wasikilize simu.
Waamrishe wajifiche kisirisiri.
Waamrishe washambulie.

d. Anataka niamrishe.
Anataka niende sasa.
Anataka nirudi leo.
Anataka niwe tayari.

e. Niamrishe?
Niende?
Nitayarishe?
Nifanye?

f. Uwe tayari.
Awe tayari.
Tuwe tayari.
Wawe tayari.

2. Semantic drills.

a. Ndege za adui.
Ndege za vita.
Ndege za msituni.

b. Eropleni za adui.
Eropleni za bomu.
Eropleni za makombora.

c. Kuwa tayari.
Kuwa macho.
Kuwa mgonjwa.

d. Kwa siri.
Kisirisiri.
Hii ni siri.

e. Simu.
Simu ya upepo.
Habari ya simu.

f. Redio.
Habari ya redio.
Redari.

g. Vidanganya macho.
Kamuflaji.
Maficho.

h. Shinda adui.
Adui ameshindwa.
Nimeshindwa kwenda.

i. Njia ya reli.
Reli ya njia mbili.
Stesheni ya reli.

j. Gari la moshi.
Kusafiri kwa gari la moshi.
Stesheni ya gari la moshi.

k. Mzinga wa ndege.
Mzinga mdogo.
Mzinga mkubwa.

l. Kuzima moto.
Kuwasha moto.
Kusikia moto.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Is the alert system working properly?

   Yes, we had a signal that enemy planes are on the way.

2. Say, does the enemy know we erected fortifications here?

   I don't know, but we must be ready (on the alert).

3. Shall I order the airmen to get ready?

   Yes, they should ready the fighter planes.

4. Will the heavy planes carry bombs?

   Not today, we will conceal ourselves here secretly.

5. Will the camouflage be enough?

   We'll know if the enemy is unable to see us.

6. There is a double track railroad nearby, also a crossroad.

   Perhaps the enemy will attack there.

7. Everyone must be ready for an attack.

   Tell the radar men to be on the alert.

8. Should the anti-aircraft gunners be ready too?

   By all means, and also the fire fighters.

LESSON 42


1
2
ADUI
3
4
5
6
7
8
!!
&

1. Mpango wa utayari unafanya kazi vizuri?
   Ndio, tumepata simu ndege za adui ni njiani.

2. Je, adui anajua tumejenga ngome hapa?
   Sijui, lakini lazima tuwe tayari.

3. Niamrishe wanahewa wajiweke tayari?
   Ndio, watayarishe ndege za vita.

4. Eropleni kubwa zitachukua makombora?
   Si leo, tutajificha hapa kisirisiri.

5. Vidanganya macho (kamuflaji) vitatosha?
   Tutajua kama adui atashindwa kutuona.

6. Kuna reli ya njia mbili karibu, hata njia panda.
   Labda adui atashambulia hapo basi.

7. Lazima wote wawe tayari kwa mashambulio?
   Waambie wenye kusimamia redari wawe macho.

8. Wenye kutumia mizinga ya ndege wawe tayari pia?
   Hasa wao, na wenye kuzima moto vilevile.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Uliniamuru nifanye kazi.
Uliniamuru nifanye kazi.

pata, maliza, tunza, anza.

b. Aliamrisha tutumie makombora.
Aliamrisha tutumie makombora.

chukua, tayarisha, peleka.

c. Kapteni aliniambia niwakamate wevi.
Kapteni aliniambia niwakamate wevi.

funga, hoji, acha, fukuza.

d. Lazima wanahewa wajitayarishe.
Lazima wanahewa wajitayarishe.

jizoeza, ondoka.

e. Waambie watumie vidanganya macho.
Waambie watumie vidanganya macho.

chukua, tafute, ondoa, weka.

f. Ninataka wenye mizinga ya ndege waondoke.
Ninataka wenye mizinga ya ndege waondoke.

kimbia, rudi, kuja, pumzika.

2. Substitution Drill

a. tufanye
Ametoa amri ------- kazi.
Ametoa amri tufanye kazi.

tafuta, uliza, pata, acha.

b. mtumie
Tumeamrisha ------ makombora.
Tumeamrisha mtumie makombora.

chukua, pata, rudisha, peleka.

c. waweke
Uliwaambia ------ ngome.
Uliwaambia waweke ngome.

haribu, vunja, ondoa, tafuta.

d. mtumie
Nimesema ------ vidanganya macho.
Nimesema mtumie vidanganya macho.

ondoa, peleka, acha, haribu.

e. wapumzike
Wenye mizinga ya ndege --------- sasa.
Wenye mizinga ya ndege wapumzike sasa.

ondoka, kwenda, simama, rudi.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning)

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the question and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Umewaambia watayarishe mpango wa utayari?
2nd: Sijawaambia watayarishe.

tengeneza, jifunza, fundisha, chungua.

b. 1st: Anataka wanahewa waondoke?
2nd: Ndio, anataka waondoke.

pumzika, lala, kuwa tayari, simama.

c. 1st: Niamrishe wenye makombora wakimbie?
2nd: Ndio, waamrishe wakimbie.

rudi, toroka, endelea, ngoja.

d. 1st: Unataka eropleni kubwa ziondoke?
2nd: Ninataka ziondoke.

simama, ngoja, pumzika, kwenda.

e. 1st: Tushambulie kwenye njia panda?
2nd: Ngojeni kwanza.

kwenda, ngoja, pumzika, tafuta.

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Umewaambia wajenge ngome?
La, sijawaambia.

tafuta, haribu, tayarisha, tengeneza.

b. Tushambulie vituo vya ndege sasa?
Ndio, shambulieni hivyo.

tafuta, jenga, tayarisha, tengeneza.

c. Nitumie mizinga ya ndege?
Ndio, tumia hiyo.

rudisha, peleka, haribu, weka.

d. Mliwarukia adui mara moja?
Tuliwazunguka kisirisiri.

shambulia, kamata, fukuza.

e. Wenye kuzima moto wamerudi?
Hawajarudi.

fika, pumzika, ondoka, kwenda.

f. Hamkutumia makombora?
Hatukutumia makombora.

pata, chukua, hitaji, peleka.

g. Watatafuta kwenye njia panda?
Hawatatafuta.

ona, ngoja, pumzika, lala.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Wakati wa vita ni lazima kujua kama adui atashambulia, ili askari wajiweke tayari. Hivi askari, hata na wenyeji wa nchi, wanafuata mpango wa utayari. Wenye kutunza mpango wa utayari wanapata habari kwa njia mbalimbali juu ya mashambulio ya adui. Halafu wanajulisha watu wetu kwa simu na njia nyingine kama adui ametoka kushambulia.

Kikosi chetu kimejenga ngome ndogo na wanajificha kisirisiri. Wametumia vidanganya macho ile adui asiwaone. Wanahewa wetu wako tayari kupigana kwa eropleni ndogo za vita, na eropleni kubwa ziko tayari hata na makombora. Lakini wanahewa watakaa tu bila kupigana, ili wamdanganye adui.

Sababu ya reli na njia panda karibu askari zetu wanafikiri adui atashambulia hapo. Ingawa ni hivyo, wote wako tayari, hata wenye kusimamia redari na wenye kuzima moto kama itatukia.

10

Step 2. Questions based on the above narration:

Ni lazima kujua nini wakati wa vita?
Mpango wa utayari ni nini?
Wenye kutunza mpango huo wanapata nini?
Wanawajulisha nani halafu?
Wanawajulisha kwa njia gani?

Kikosi chetu kimejenga nini?
Wanajificha wapi?
Wametumia nini?
Wanahewa wako tayari kufanya nini?
Eropleni kubwa zinachukua nini?

Wanahewa watakaa kisirisiri?
Watapigana kama ni lazima?
Kuna nini karibu?
Askari wanafikiri nini?
Nani tena ni tayari?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 43

LESSON 43



1st PERIOD PERCEPTION DRILL LESSON 43

Note: The situational picture will be used as an aid
during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension..

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on the indirect command.

   a. Asugue vifungo.
      Asugue mshipi.
      Asugue alama za cheo.

   b. Waambie wakazane.
      Waambie wasafishe.
      Waambie wapange.

2. Drill on imperatives with future tense.

   a. Watakunja mablanketi.
      Watakunja nguo.

   b. Watatundika mablanketi.
      Watatundika kabuti.

   c. Watapiga pasi shati.
      Watapiga pasi kaptula.

   d. Watanyunyiza dawa.
      Watanyunyiza diditii.

   e. Watapiga polishi viatu.
      Watapiga polishi mshipi.

   f. Tutachoma takataka.
      Tutafagia takatal.

3. Semantic drills.

a. Chawa ni mdudu.
Kunguni ni mdudu.

b. Mainzi ni wadudu.
Mbu ni wadudu.

c. Dawa ya kuua wadudu.
Diditii ni dawa kali.
Diditii ni dawa sumu.

d. Anakwenda choo.
Anasafisha choo.
Anafagia choo.

e. Watapanga kila kitu.
Kila kitu kitapangwa.

f. Kifungo cha koti.
Kifungo cha kabuti.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Sgt.! The commander will inspect camp today.

   Very well, Sir, everything will be in good order.

2. Pass through the barracks and inspect the beds.

   They'll fold the blankets and arrange the equipment.

3. Each soldier will polish buttons, insignia and belt (buckles).

   They'll polish everything, including the boots.

4. They'll iron the pants, shirts and coats too.

   And they'll hang up their overcoats properly.

5. Spray some DDT everywhere.

   This is potent stuff for killing insects, isn't it?

6. Yes, it will kill mosquitoes, lice and bed bugs.

   We'll use it in the latrines to kill flies too.

7. Those detailed to clean latrines and sweep the grounds better do their best.

   Yes, Sir, I'll follow your instructions.

8. Warn the cook to clean the kitchen well.

   O.K., and we'll burn the rubbish outside of camp.

LESSON 43


1
!
+++
2
3
4
&
!!
&
5
Di
Di
Tii
DDT
6
7
!
8
ok
&

1. Sajini! Kamanda atakagua kambi leo.
   Vizuri, Effendi, kila kitu kitapangwa sawasawa.

2. Pitia katika vibanda na kagua vitanda.
   Watakunja mablanketi na kupanga mabeti.

3. Kila askari asugue vifungo, alama za cheo na mishipi.
   Watapiga polishi kila kitu, hata viatu.

4. Watapiga pasi kaptula, shati na koti vilevile.
   Na watatundika kabuti zao sawasawa.

5. Nyunyiza dawa ya diditii (DDT) popote.
   Hii ni dawa kali ya kuua wadudu, sivyo?

6. Ndivyo, itaua mbu, chawa na kunguni.
   Tutatumia chooni kuua mainzi pia.

7. Wenye kufagia choo na kiwanja wakazane.
   Ndio, Effendi, nitafuata amri zako.

8. Mwonye mpishi asafishe jikoni vizuri.
   Vizuri, hata takataka tutachoma nje ya kambi.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Kamanda ametuamuru tutayarishe silaha.
Kamanda ametuamuru tutayarishe silaha.

weka, safisha, rudisha, ficha.

b. Lazima askari wasugue vifungo.
Lazima askari wasugue vifungo.

chukua, shona, tengeneza, tunza.

c. Waambie wanyunyize diditii popote.
Waambie wanyunyize diditii popote.

tia, tumia.

d. Mwonye mpishi asafishe jiko.
Mwonye mpishi asafishe jiko.

tayarisha, fagia, panga.

e. Nimemwambia afagie choo.
Nimemwambia afagie choo.

safisha, tumia, jenga.

f. Kamanda atakagua kambi leo.
Kamanda atakagua kambi leo.

tembelea, ingia, angalia.

2. Substitution Drill

a. apitie
Mwambie ------ hapa.
Mwambie apitie hapa.

fagia, ingia, toka, kuja.

b. tukunje

Ametuamrisha ------- mablanketi.

Ametuamrisha tukunje mablanketi.

safisha, leta, tumia, nunua.

c. upige pasi

Nilikuamuru ----- ---- kaptula na shati.

Nilikuamuru upige pasi kaptula na shati.

tayarisha, rudisha, panga, weka.

d. mtundike

Sajini amesema -------- kabuti sawasawa.

Sajini amesema mtundike kabuti sawasawa.

safisha, weka, tunza, vaa.

e. mtumie

Ninataka ------ diditii kuua wadudu.

Ninataka mtumie diditii kuua wadudu.

nunua, tafuta, pata, leta.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 43

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the question and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Umemwambia akague kambi?
2nd: Sijamwambia akague.

ingia, tafuta, tunza.

b. 1st: Wamepanga mablanketi na mabeti?
2nd: Nimewaambia wapange vyote.

nunua, safisha, leta, rudisha.

c. 1st: Alitumia diditii kuua mbu na chawa?
2nd: Nilimwonya atumie diditii.

nunua, leta, chukua, peleka.

d. 1st: Alisema tufagie choo?
2nd: Ndio, alisema mfagie choo.

tumia, tafuta, jenga, safisha.

e. 1st: Uliwaambia wachome takataka?
2nd: Ndio, niliwaambia.

ondoa, chukua.

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Wamepanga mabeti yao?
   Tumewaambia wapange mabeti.

   safisha, peleka, uza, leta.

b. Amekagua vitanda?
   Nimemwamrisha akague vitanda.

   panga, chukua, safisha, tunza.

c. Mlipata amri kutundika kabuti?
   Tulipata amri tutundike kabuti.

   chukua, uza, tunza, leta.

d. Kapteni aliamrisha tuwavizie adui?
   Ndio, aliamrisha tuwavizie adui.

   kamata, fukuza, hoji, haribu.

e. Alisema mtumie makombora?
   Ndio, alisema tutumie makombora.

   nunua, peleka, haribu, weka.

f. Alikuonya usafishe nyumba?
   Ndio, alinionya nisafishe nyumba.

   ingia, toka, fagia, bomoa.

g. Alisema mjifiche kando ya njia?
   Ndio, alisema tujifiche huko.

   kaa, simama, ngoja, lala.

6th PERIOD SITUATIONAL APPLICATION LESSON 43

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Kamanda ni ofisa mkubwa. Yeye anapokagua kambi ni lazima kila kitu kuwa sawasawa kabisa. Kamanda atakuja leo na Sajini anatayarisha watu wote.

Askari katika vibanda wanatengeneza vitanda vizuri na wanakunja mablanketi sawasawa. Kila askari anasugua vifungo na mishipi, na wanapiga polishi viatu vyao vyeusi. Halafu watapiga nguo zao pasi, hasa kaptula, shati na koti. Watatundika kabuti juu ya vitanda.

Koplo atatoa amri kunyunyiza dawa ya diditii popote kuua wadudu kama chawa, kunguni, mainzi na mbu. Katika choo kuna mainzi wengi. Diditii ni dawa kali sana na sumu. Ni lazima kutumia dawa hiyo taratibu ili watu wasipate ugonjwa. Wenye kufagia kiwanja wanasafisha choo vilevile. Hiyo si kazi nzuri, lakini ni lazima kwa afya.

Mpishi atasafisha jikoni na atachoma takataka nje ya kambi.

Step 2. Questions based on the above narration:

Kamanda ni ofisa mdogo?
Atafanya nini leo?
Sajini anafanya nini sasa?
Askari wanafanya nini katika vibanda?
Nani anakunja mablanketi?

Kila askari anafanya nini na vifungo?
Wanapiga nini polishi?
Watafanya nini na nguo zao?
Kaptula, shati ni nguo za Askari?
Watatundika kabuti wapi?

Koplo atatoa amri kunyunyiza nini?
Diditii ni dawa gani?
Ni dawa ya kuua nini?
Mainzi wengi wako wapi?
Mpishi atafanya nini?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 44

LESSON 44



1st PERIOD PERCEPTION DRILL LESSON 44

Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on personal relative pronouns.

a. Anayevaa shati.
Aliyefungua mkutano.
Atakayefungua mkutano.

b. Waliokutanika.
Waliobaki.
Waliotoka.

c. Anayepaaza sauti.
Anayeketi.
Anayesimama.

d. Watakaokwenda.
Watakaofanya.
Watakaohutubu.

2. Semantic drills.

a. Mwenye kiti.
Mwenye kusema.
Mwenye sauti.
Mwenye neno.

b. Mwandishi.
Mwandishi mdogo.
Mwandishi anaandika.
Kitabu cha mwandishi.

c. Umati wa watu.
Umati mkubwa.
Umati wa wanachama.
Umati uliokutanika.

d. Fungua mkutano.
Ongoza mkutano.
Komesha mkutano.
Hudhuria mkutano.

e. Sauti kubwa.
Sauti ndogo.
Paaza sauti.

f. Wanachama waliotangulia.
Wanachama waliobaki.
Wanachama walioondoka.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

2nd PERIOD ENGLISH DIALOGUE LESSON 44

1. What are the people who are gathering there waiting for?

   They are waiting for the chairman of their society.

2. Who is that one wearing a brown shirt?

   That is the assistant secretary of the society.

3. The leaders are arriving; who are the ones who will speak?

   Those who will speak are taking their seats now.

4. Who will open the meeting?

   The chairman will open the meeting.

5. Is that he who opened the meeting last Sunday?

   Yes, watch him, he has a long moustache.

6. The meeting is beginning; will the noisemakers shut up?

   All will be quiet after a few minutes.

7. Will the crowd disperse after the meeting?

   Yes, the members who came from far away will return home.

8. Will others remain in town?

   Those who remain in town will leave tomorrow.

LESSON 44

1



2


KARANI MDOGO

3



4


MWENYE KITI

5



6



7



8



1. Watu wanaokutanika pale wanangojea nini?
Wanamngojea mwenye kiti wa chama chao.

2. Yule anayevaa shati ya hudhurungi ni nani?
Huyo ni mwandishi mdogo wa chama.

3. Viongozi wanafika; watakaohutubu ni nani?
Watakaohutubu wanashika viti vyao sasa.

4. Atakayefungua mkutano ni nani?
Mwenye kiti atafungua mkutano.

5. Ni yeye aliyefungua mkutano Jumapili iliyopita?
Ndio, mwangalie vizuri, ana masharubu marefu.

6. Mkutano unaanza; wanaopiga kelele watanyamaza?
Wote watakaa kimya baada ya dakika chache.

7. Baada ya mkutano umati utatawanyika?
Ndio, wanachama waliotoka mbali watarudi kwao.

8. Wengine watabaki mjini?
Watakaobaki mjini wataondoka kesho.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Kijana anayekuja ni mwalimu.
Kijana anayekuja ni mwalimu.

lima, simama, soma, kimbia.

b. Watu wanaopigana ni askari.
Watu wanaopigana ni askari.

rudi, tembea, ingia, ondoka.

c. Daktari aliyeondoka amerudi.
Daktari aliyeondoka amerudi.

faulu, anguka, toroka, hutubu.

d. Viongozi waliohutubu wameondoka.
Viongozi waliohutubu wameondoka.

simama, kuja, pumzika, fanya kazi.

e. Mwanamke atakayelima anaongea.
Mwanamke atakayelima anaongea.

shindana, saidia, fagia, andika.

2. Substitution Drill

a. waliongojea
Wakulima ---------- watafaulu.
Wakulima waliongojea watafaulu.

kutanika, hutubu, andika, burudika.

b. atakayechelewa
Mvuvi ------------- ataonekana.
Mvuvi atakayechelewa ataonekana.

iba, toroka, lalamika, rudi.

c. anayefundisha
Mwalimu ------------ ni mkubwa.
Mwalimu anayefundisha ni mkubwa.

lala, kagua, winda, ngojea.

d. waliorudi
Wanawake --------- wataondoka.
Wanawake waliorudi wataondoka.

pumzika, pika, shindana, tazama.

e. wanaowinda
Wenyeji ---------- wanafurahi.
Wenyeji wanaowinda wanafurahi.

cheza, safiri, saidia, simama.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 44

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the question and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Wanachama waliokutanika walisongana?
2nd: Walisongana sana.

ingia, sikiliza, simama, keti.

b. 1st: Atakayefungua mlango ni nani?
2nd: Atakayefungua mlango ni mpelelezi.

vunja, funga, bomoa, choma.

c. 1st: Mswahili anayeketi ni Ali?
2nd: Mswahili anayeketi si Ali.

lima, lala, tazama, kimbia.

d. 1st: Wakulima watakaorudi watafurahi?
2nd: Ndio, watafurahi.

burudika, abudu, safiri, faulu.

e. 1st: Ulimwona simba aliyekufa?
2nd: Ndio, nilimwona huyo.

kimbia, ruka, simama, lala.

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Nani aliyekupiga?
Aliyenipiga ni mwivi.

tuma, ita, hoji, taja.

b. Watakaoshindana wamefika?
Hawajafika wote.

safiri, shambulia, winda, fanya kazi.

c. Watoto wanaosoma ni wavivu?
Watoto wanaosoma si wavivu.

cheza, kimbia, lala, piga kelele.

d. Watu walioshindwa wameondoka?
Walioshindwa wameondoka wote.

iba, lala, pumzika, shinda.

e. Wakili atakayefaulu anasoma?
Ndio, anasoma sasa.

ondoka, pumzika, umia, fika.

f. Mtu anayelala ni mwalimu?
Ndio, ni mwalimu.

simama, kimbia, cheka, tembea.

g. Mwivi aliyetoroka ni huyu?
Ndio, ni huyo.

iba, ingia, ruka, jificha.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Tazama umati mkubwa wa wanaume na wanawake kule kiwanjani. Wamekutanika leo kumsikiliza kiongozi wa chama. Watu waliokutanika ni wanachama wa chama cha biashara. Sasa wanamngojea mwenye kiti afungue mkutano.

Yule anayeketi sasa ni mwenye kiti. Yeye ni kiongozi hodari. Mwandishi ni yule anayevaa shati rangi hudhurungi. Wengine wanaosimama karibu ni viongozi wengine vema.

Wote wanaosema kwa sauti kubwa na kupiga kelele sasa watanyamaza. Watakaa kimya mwenye kiti atakapofungua mkutano, na atakapopaaza sauti yake.

Baada ya mkutano watu waliotoka mbali watabaki na watalala mjini usiku. Wanaokaa karibu watatangulia kuondoka leo. Hivi wote watatawanyika upesi. Mwandishi aliyeandika habari za mkutano kitabuni atabaki kusema na mwenye kiti.

Step 2. Questions based on the above narration:

Waliokutanika ni nani?
Umati wa watu ni watu wachache?

Watu wamekutanika wapi?
Waliokutanika ni wanachama?
Wanamngojea nani?

Mwenye kiti atafanya nini?
Anayeketi ni nani?
Nani hodari?
Nani anavaa shati hudhurungi?
Wanaosimama karibu ni nani?

Watu wanasema kwa sauti ndogo?
Watanyamaza baadaye?
Nani atapaaza sauti?
Waliotoka mbali watalala wapi?
Mwandishi atafanyaje?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

ED026651

DEFENSE LANGUAGE INSTITUTE

WEST COAST BRANCH

PRESIDIO OF MONTEREY, CALIFORNIA

SWAHILI

12 WEEKS COURSE

VOLUME V
LESSONS 45-55

РУССКИЙ
СРПСКОХРВАТСКИ
華 語
SHQIP
MAGYAR
日 本 語
TÜRKÇE
PORTUGUÊS
فارسی
ROMÂNĂ
УКРАЇНСЬКА
ITALIANO
BAHASA INDONESIA
ภาษาไทย

БЪЛГАРСКИ
POLSKI
粤 語
ČESKY
ΕΛΛΗΝΙΚΑ
한 국 어
ESPAÑOL
FRANÇAIS
العربية
SLOVENŠČINA
မြန်မာဘာသာ
DEUTSCH
TIẾNG VIỆT NAM
LIETUVIŲ

KISWAHILI

AL 001 753

SWAHILI

12 WEEKS COURSE

Volume V

Lessons 45-55

March 1963

DEFENSE LANGUAGE INSTITUTE
West Coast Branch
Presidio of Monterey, California

CONTENTS

Page

LESSON 45 657

LESSON 46 671

LESSON 47 685

LESSON 48 699

LESSON 49 713

LESSON 50 727

LESSON 51 743

LESSON 52 757

LESSON 53 771

LESSON 54 785

LESSON 55 799

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 45

LESSON 45



Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on the 'A' tense.

a. Nataka tochi.
Nafuata njia.
Nachukua taa.
Nakumbuka kila mara.

b. Twalazimiwa kupita.
Twaondoka sasa.
Twahitaji jiko.
Twajaribu gari.

c. Mwakumbuka taa.
Mwajaza petroli.
Mwafahamu amri.
Mwaangalia fanusi.

d. Wafanya nini siku hizi?
Wajaribu kufika?
Watengeneza kahawa?
Wafahamu saa ya kuondoka?

2. Semantic drills.

a. Jaza tangi!
Jaza kikapu!
Jaza sanduku!

b. Tangi ya maji.
Tangi ya petroli.
Tangi ya mafuta.

c. Umefahamu nini?
Umekumbuka nini?
Umewasha nini?

d. Nuru ya taa.
Nuru ya jua.
Nuru ya mwezi.

e. Punguza kidogo.
Punguza petroli.
Punguza watu.

f. Usiku sana.
Usiku saa sita.
Usiku wa manane.

g. Giza tupu.
Maji tupu.
Ukungu tupu.

h. Endesheni kwa uangalifu.
Endesheni polepole.
Endesheni upesi.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Do we have to pass through enemy territory at night?

   Yes, it will be dangerous to show a light.

2. Corporal, do you understand that we leave at eight p.m.?

   I understand, Sir, we are filling the tanks with gas now.

3. Are you remembering to check the lights on the vehicles?

   Yes, but the moonlight will be sufficient.

4. All of you must try to get there before midnight.

   True, the mist (fog) will be heavy at that time too.

5. Are all soldiers ordered to carry a torch (flashlight)?

   Yes, but they may not flash a torch without permission.

6. Take lanterns and sufficient kerosene.

   Yes, it will be completely dark when we get to camp.

7. Do we need a stove for fixing coffee at night?

   No, carry the coffee in canteens.

8. Let every driver remember to drive with care.

   All the drivers know their job.

LESSON 45

1



2



3



4



5


??
!
BILA RUHUSA

6



7



8



1. Twalazimiwa kupitia nchi ya adui usiku?

Ndio, itakuwa hatari kuonyesha nuru ya taa.

2. Koplo, wafahamu twaondoka saa mbili usiku?

Nafahamu, Effendi, twajaza matangi na petroli sasa.

3. Mwakumbuka kuangalia taa za magari?

Ndio, lakini nuru ya mwezi itatosha.

4. Jaribuni kufika kabla ya usiku wa manane.

Kweli, hata ukungu utazidi wakati huo.

5. Askari wote waamrishwe kuchukua tochi?

Ndio, lakini wasiwashe tochi bila ruhusa.

6. Chukueni fanusi na mafuta ya taa ya kutosha.

Ndio, itakuwa giza tupu tutakapofika kambini.

7. Twahitaji jiko kwa kutengeneza kahawa usiku?

La, chukueni kahawa katika vibuyu.

8. Kila dereva akumbuke kuendesha kwa uangalifu.

Madereva wote wajua kazi yao.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Twalazimiwa kuondoka sasa.
Twalazimiwa kuondoka sasa.

taka, amrishwa, furahi, tayarisha.

b. Afahamu kuangalia taa zote.
Afahamu kuangalia taa zote.

kumbuka, tumaini, taka, endelea.

c. Natazama matangi ya petroli.
Natazama matangi ya petroli.

tengeneza, haribu, toboa, jaza.

d. Mwazidi kuharibu gari.
Mwazidi kuharibu gari.

taka, tumaini, jaribu, penda.

e. Wahitaji tochi sasa.
Wahitaji tochi sasa.

tumia, chukua, haribu, tengeneza.

f. Nakumbuka kuwauliza.
Nakumbuka kuwauliza.

tumaini, taka, furahi, fika.

2. Substitution Drill

a. Alazimiwa
--------- kuingia hapa.
Alazimiwa kuingia hapa.

taka, tumaini, tamani, furahi.

b. Mwakumbuka
---------- kuwasha taa.
Mwakumbuka kuwasha taa.

fahamu, amrishwa, weza, jua.

c. Twatengeneza
------------ matangi haya.
Twatengeneza matangi haya.

uza, nunua, jaza, leta.

d. Nazidi
------ kuendesha gari.
Nazidi kuendesha gari.

taka, jua, endelea, weza.

e. Twahitaji
--------- mafuta ya taa.
Twahitaji mafuta ya taa.

nunua, uza, peleka, tumia.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 45

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the question and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Walazimiwa kuuza gari?
2nd: Ndio, nalazimiwa kuuza gari.

tumaini, taka, ngojea, fikiri.

b. 1st: Mwakumbuka kuwasha taa?
2nd: Ndio, twakumbuka hivi.

jua, penda, taka, tumaini.

c. 1st: Waendelea kutengeneza gari?
2nd: Ndio, naendelea kutengeneza gari.

taka, tayarisha, fikiri, penda.

d. 1st: Wahitaji mafuta gani?
2nd: Nahitaji mafuta ya taa.

taka, nunua, tafuta, penda.

e. 1st: Akumbuka kuwauliza?
2nd: Ndio, akumbuka.

tumaini, furahi, chelewa, hitaji.

RECOMBINATION DRILL

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Mwajua kuendesha gari?
Hatujui kuendesha gari.

tamani, jaribu, tumaini, penda.

b. Ataka kwenda nyumbani?
Ndio, atataka kwenda huko.

ngoja, fikiri, kataa, penda.

c. Watafuta kitu gani?
Natafuta tochi.

nunua, uza, peleka, tumia.

d. Twaanza kusafiri sasa?
Ndio, twaanza kusafiri.

tumaini, acha, endelea, taka.

e. Mwajizoeza kambini?
La, twajizoeza kiwanjani.

tembea, rudi, enda, kutana.

f. Waingia mjini?
La, waingia msituni.

lala, kaa, fanya kazi, jificha.

g. Afagia nyumba?
La, afagia gari.

nunua, taka, uza, tafuta.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Kwa ghafula Kapteni aliamuru kikosi chake wakati wa jioni ya kwamba hawatakaa kambini usiku. Watalazimiwa kupitia nchi ya adui usiku. Hiyo ni hatari kwa sababu ya adui wengi, na kusafiri katika giza ya usiku bila taa.

Koplo alitayarisha magari, alitia petroli katika matangi, na aliangalia kama taa zote zaweza kuwaka. Nuru ya mwezi itawasaidia kusafiri usiku na kupunguza giza. Lakini ni lazima wasafiri upesi ili wafike katika kambi ya pili kabla ya usiku wa manane. Wakati huo ukungu waweza kuzidi na kuleta shida.

Kila askari atachukua tochi yake na kibuyu na kahawa moto. Hawawezi kutumia tochi hizo bila ruhusa. Panusi itawafaa watakapofika kambini. Madereva wote walionywa kuendesha kwa uangalifu sana.

Step 2. Questions based on the above narration:

Kapteni aliamuru nini?
Kikosi kitalala kambini?

Kikosi kitapitia wapi?
Kuna hatari gani hapo?
Watasafiri gizani bila taa?

Nuru gani itasaidia gizani?
Koplo alitayarisha nini?
Alitia nini katika matangi?
Ni lazima wasafiri upesi?
Watafika kambi ya pili lini?

Ukungu utaweza kuzidi wakati gani?
Kila askari atapata tochi vilevile?
Atatumia tochi bila ruhusa?
Fanusi itawafaa wapi?
Madereva wataendesha namna gani?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 46


GEREJI

1st PERIOD PERCEPTION DRILL LESSON 46

Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on the 'HU' tense.

a. Motokaa huharibika.
Motokaa huwaka upesi.
Motokaa hupendeza.

b. Mekanika huaminika.
Mekanika hutengeneza.
Mekanika hufanya kazi.

c. Ndege huruka.
Ndege hula chakula.
Ndege hukaa pale.

d. Watoto hucheza.
Wanafunzi hujifunza.
Walimu hufundisha.

e. Dereva huendesha motokaa.
Mwanahewa huendesha eropleni.
Wao huendesha mtumbwi.

f. Askari hodari hupigana.
Wanyama hula majani hapa.
Simba huua swala.

2. Semantic drill on borrowed words.

a. Anasafisha karbureta.
Anasafisha plagi.
Anasafisha injini.

b. Anajaza redieta.
Anajaza beteri.
Anajaza tangi.

c. Badilisha mafuta ya injini.
Badilisha mafuta ya gia.
Badilisha mafuta ya taa.

d. Hupiga ripoti.
Hupiga stati.
Hupiga pasi.

e. Tumehakikisha.
Tumebadilisha.
Tumepima tairi.

f. Anatia girisi.
Anatia petroli.
Anatia mafuta.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Where's the garage? The car is breaking down all the time.

   The garage is over there, and the mechanics are reliable.

2. How are y'all? Are you the mechanics here?

   Yes, we work here all the time.

3. My car won' go! Please clean the carburetor.

   O.K., we'll check the battery too.

4. The car usually starts up quickly.

   But now it won't?

5. Yes, make sure the wiring and plugs are O.K.

   The plugs get worn out quickly these days.

6. Afterwards change the oil in the engine.

   O.K. and we'll test the tires too.

7. Change the gear oil and grease it everywhere.

   O.K., I'll also see if the radiator is full.

8. When you finish the job, fill up the tank with gas.

   We'll fix everything right.

LESSON 46


1
GEREJI
?
GEREJI
2
?
??
V,
3
4
+/-
!??X
5
V,
6
&
7
8
??

1. Wapi gereji? Motokaa huharibika kutwa.
   Gereji ni pale, na mekanika huaminika.

2. Hamjambo? Ninyi ni mekanika hapa?
   Ndio, twafanya kazi hapa siku zote.

3. Gari langu haliendi! Tafadhali safisha kabureta.
   Vizuri, tutaangalia beteri pia.

4. Motokaa huwaka upesi ninapopiga stati.
   Lakini sasa inakataa?

5. Ndio, hakikisha kama waya na plagi ni nzuri.
   Plagi huharibika upesi siku hizi.

6. Halafu badilisha mafuta katika injini.
   Vema na tutapima tairi vilevile.

7. Badilisha mafuta ya gia na tia girisi popote.
   Vema, nitahakikisha redieta imejaa vilevile.

8. Utakapomaliza kazi, jaza tangi petroli.
   Tutatengeneza kila kitu sawasawa.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Motokaa huharibika kutwa.
   Motokaa huharibika kutwa.

   enda, simama, tengenezwa, saidia.

b. Gari langu haliendi.
   Gari langu haliendi.

   simama, haribika, faa.

c. Plagi huharibika upesi.
   Plagi huharibika upesi.

   pasuka, vunjika,

d. Mtoto huyu huaminika sana.
   Mtoto huyu huaminika sana.

   fanya kazi, pumzika, lala, jifunza.

e. Mekanika hubadilisha mafuta siku zote.
   Mekanika hubadilisha mafuta siku zote.

   ongeza, tia, tumia, pata.

2. Substitution Drill

a. huharibika
   Mashine ---------- mara nyingi.
   Mashine huharibika mara nyingi.

   vunjika, simama.

b. hutengeneza
Mekanika ----------- plagi siku zote.
Mekanika hutengeneza plagi siku zote.

nunua, haribu, uza, rudisha.

c. huaminika
Mtu huyu --------- kila mara.
Mtu huyu huaminika kila mara.

jifunza, fundisha, lala, pumzika.

d. huendesha
Dereva --------- motokaa kila siku.
Dereva huendesha motokaa kila siku.

leta, tengeneza, safisha.

e. hupasuka
Plagi -------- kila mara.
Plagi hupasuka kila mara.

haribika, vunjika, chomeka.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 46

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the question and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Motokaa huharibika kila mara?
2nd: Ndio, huharibika kila mara.

simama, chafuka, vunjika, kutana.

b. 1st: Mashine hii huharibika saa zote?
2nd: La, huharibika mara chache tu.

simama, pendeza, pinduka, waka.

c. 1st: Mekanika huyu hufanya bidii sana?
2nd: Ndio, hufanya bidii sana.

kazana, chelewa, aminika, pumzika.

d. 1st: Redieta yako hupasuka mara nyingi?
2nd: La, haipasuki mara nyingi.

vunjika, toboka, haribika.

e. 1st: Dereva hubadilisha mafuta kila siku?
2nd: Ndio, hubadilisha mafuta kila siku.

nunua, uza, pata, tafuta.

5th PERIOD RECOMBINATION DRILL LESSON 46

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Waislamu huabudu Jumapili?
La, huabudu Ijumaa.

kutanika, burudika, pumzika.

b. Wavuvi hupenda kuvua samaki?
Ndio, hii ni kazi yao.

furahi, enda, ondoka, tamani.

c. Daktari huyu hupumzika Jumapili?
Ndio, hupumzika kila Jumapili.

fanya kazi, burudika, ogelea, tembea.

d. Wagonjwa hulalamika siku zote?
Wengine hawalalamiki.

umia, pata dawa, pumzika, lala.

e. Adui hushambulia kila jioni?
La, hawashambulii kila siku.

ingia, tawanyika, kutanika, hama.

f. Hakimu hutoa hukumu siku zote?
Siku nyingine hatoi hukumu.

chelewa, rudi, jifunza, amua kesi.

g. Wakulima huvuna kila mwezi?
La, hawavuni kila mwezi.

panda, lima, kata miti, fyeka.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Juzi nilisafiri kwa motokaa kuonana na daktari. Motokaa yangu ni mzee kidogo na siku hizi ilianza kufanya matata. Hivyo nilipopita mjini nilitafuta gereji. Mtu mmoja aliniambia niende kwa gereji moja hapo karibu. Alisema mekanika ni hodari na anaaminika.

Mekanika aliyekuwa hapo aliniamkia na aliuliza habari ya motokaa. Nilimwambia asafishe kabureta na ahakikishe kama waya na plagi zote ni sawasawa. Atakapomaliza kazi hiyo nilitaka abadilishe mafuta katika injini na atie girisi, vilevile aangalie redieta, beteri na tairi zote.

Mekanika alitengeneza kila kitu vizuri. Nilipopiga stati injini iliwaka maramoja. Nilifurahi, nilimpa pesa zake, na niliendelea safari kuonana na daktari kwa sababu ya ugonjwa.

Step 2. Questions based on the above narration:

Nilikwenda wapi juzi?
Motokaa yangu ni mpya?
Ilianza kufanya matata?
Nilitafuta nini mjini?
Mekanika katika gereji alikuwa mtu mwema?

Nani aliniamkia?
Nilitaka mekanika asafishe nini?
Atafanya nini na plagi?
Nilitaka abadilishe mafuta?
Vilevile nilitaka aangalie nini?

Mekanika alitengeneza motokaa sawasawa?
Injini iliwaka upesi?
Nani alifurahi?
Niliendelea kuonana na nani?
Nilitaka kuonana na daktari sababu gani?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 47

LESSON 47



Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on the 'NGE' tense.

a. Tungeokoka.
Tungemwuliza.
Tungefika.
Tungepotea.

b. Angeelekeza.
Angetuambia.
Angezama.
Angeokoka.

c. Wangefanya bidii.
Wangezamishwa.
Wangeogelea.
Wangetumia.

d. Ningependa.
Ningekuwa.
Ningefurahi.
Ningempa.

e. Ungefurahi?
Ungesafiri?
Ungetumia?
Ungemwuliza?

f. Mngeingia?
Mngefika?
Mngeogelea?
Mngetulia?

2. Semantic drills.

a. Dhoruba kali.
Dhoruba baharini.
Dhoruba imeingia.

b. Nahodha hodari.
Nahodha wa meli.
Nahodha angeelekeza.

c. Bandari ya meli.
Bandari gani?
Kuingia bandarini.

d. Baharia angeogelea.
Baharia hodari.
Mabaharia wa meli.

e. Meli ingezama.
Meli inachukua abiria.
Meli inapita baharini.

f. Papa ni samaki mkubwa.
Papa anakula watu.
Papa anatafuna watu.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

2nd PERIOD ENGLISH DIALOGUE LESSON 47

1. A heavy storm is upon us, what shall we do?

   If the captain would head the ship into port we'd be saved.

2. What distance are we from a harbor?

   If we'd ask the captain he'd tell us.

3. If the sailors would try hard would we reach the shore?

   We would reach the shore without danger.

4. If the ship would go down now would we be lost?

   We'd get saved if we'd use life boats.

5. Would one boat be enough for all?

   No, the sailors would swim to shore.

6. Would others be drowned by the waves?

   Yes, for this is a very heavy storm.

7. If the ocean were calm would they be safe swimming?

   The sharks would get many before they reached shore.

8. Truly, if I were on shore I'd be happy.

   Likely we'll succeed in getting there.

LESSON 47


1
?!
2
?
??
3
?!?
4
??
5
??
1
X,
6
??
✓,
7
??
8

1. Dhoruba kali imeingia, tutafanya nini?
   Nahodha angeelekeza meli hii bandarini tungeokoka.

2. Tuko umbali gani kutoka bandari?
   Tungemwuliza nahodha angetuambia.

3. Mabaharia wangefanya bidii tungefika pwani?
   Tungefika pwani bila hatari.

4. Kama meli hii ingezama sasa tungepotea?
   Tungeokoka kama tungetumia mashua.

5. Mashua moja ingetutosha wote?
   La, mabaharia wangeogelea pwani.

6. Wengine wangezamishwa na mawimbi ya maji?
   Ndio, kwani dhoruba hii ni kubwa mno.

7. Bahari ingetulia wangeogelea salama?
   Papa wangewatafuna wengi kabla ya kufika pwani.

8. Kweli, ningekuwa pwani ningefurahi.
   Pengine tutafaulu kurudi kule.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Kama angeingia angekufa.
Kama angeingia angekufa.

gongwa, chelewa, onekana, karibia.

b. Kama ningekazana ningefaulu.
Kama ningekazana ningefaulu.

lalamika, tangulia, vumilia, kumbuka.

c. Kama ungelipa ungeokoka.
Kama ungelipa ungeokoka.

kumbuka, fuatana, hama, ongoza.

d. Kama wangeogelea wangefika pwani.
Kama wangeogelea wangefika pwani.

tumia mashua, amini, kata neno, tawanyika.

e. Kama tungeelekea pwani tungefurahi.
Kama tungeelekea pwani tungefurahi.

acha, karibia, kutana, ingia.

f. Kama mngefahamu mngeamini.
Kama mngefahamu mngeamini.

pata alama, kutanika, elezewa, abudu.

2. Substitution Drill

a. wangemwuliza
Kama ----------- angewaambia.
Kama wangemwuliza angewaambia.

tafuta, pata, amini, fuata.

b. ningekufahamu
Kama ------------- ningekushauri.
Kama ningekufahamu ningekushauri.

amini, ita, kagua, ongoza.

c. angenitisha
Kama ----------- angeniumiza.
Kama angenitisha angeniumiza.

shtaki, tambua, vizia, sukuma.

d. ungewaonya
Kama ---------- wangehudhuria.
Kama ungewaonya wangehudhuria.

pendeza, onyesha, lipa, fuata.

e. tungewasalimieni
Kama ---------------- mngelalamika.
Kama tungewasalimieni mngelalamika.

ruhusuni, sukumeni, kopesheni, umizeni.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 47

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the question and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Dhoruba ingeingia tungeangamia?
2nd: Tungeangamia wote.

potea, zama, kata tamaa, tawanyika.

b. 1st: Nahodha angeelekea pwani mngefurahi?
2nd: Tungefurahi kweli.

faulu, burudika, okoka, chelewa.

c. 1st: Meli hii ingezama wangekufa?
2nd: Wangekufa mara moja.

pasuka, pinduka, gongwa, vunjika.

d. 1st: Mashua ingepinduka ungekata tamaa?
2nd: Ningeogelea pwani.

okoka, ogelea, kufa, fanya nini.

e. 1st: Papa angekuona angekutafuna?
2nd: Kweli, angenitafuna.

umiza, kamata, jeruhi.

5th PERIOD RECOMBINATION DRILL LESSON 47

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Kama angekuja mngetoroka?
Tungetoroka wote.

tawanyika, vumilia, onekana, chelewa.

b. Kama tungemwita angesikia?
Angesikia bila shaka.

geuka, fahamu, okoka, hudhuria.

c. Kama mngekazana mngefaulu?
Tungekazana tungefaulu.

fahamu, umia, fika, burudika.

d. Kama ungewapendeza wangekuamini?
Ndio, wangeniamini.

ruhusu, salimia, fuata, tunza.

e. Kama wangekata neno wangetuona?
Wangekata neno wangetuona.

shtaki, sukuma, elekea, ongoza, lisha.

f. Kama ningekusalimia ungenipenda?
Ndio, ningekupenda.

tambua, amini, fuata, karibia.

g. Kama angekufuata ungeogopa?
Angenifuata ningeogopa.

kimbia, okoka, lalamika, kata tamaa.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Tuliposafiri baharini katika meli moja ya Kiingereza dhoruba kali iliingia. Abiria wote waliogopa sana kwamba meli itazama. Abiria mmoja aliona kama nahodha angeelekea bandarini wangeokoka. Lakini sasa hawakujua bandari uko umbali gani. Kama wangemwuliza mahodha labda angewaambia. Wengine walifikiri labda mabaharia wangefanya bidii wangefaulu kufika pwani. Wengine tena waliuliza kama mashua ingetosha kwa wote, lakini waliona kwamba haingetosha. Mabaharia wangelazimishwa kuogelea majini. Mawimbi yalikuwa makubwa na papa wangetafuna wengi kabla ya kufika pwani.

Sasa abiria wengi walisema wangefurahi sana kuwa pwani. Lakini sisi tuliamini kwamba tutafaulu kufika pwani salama.

Step 2. Questions based on the above narration:

Tulisafiri wapi?
Tulisafiri katika meli gani?
Nini iliingia halafu?
Abiria walifurahi?
Abiria waliogopa nini?

Mmoja alitaka nahodha afanyeje?
Walijua bandari uko umbali gani?
Nahodha angewaambia?
Wangefaulu kufika pwani kama mabaharia wangefanya bidii?
Mashua ingetosha kwa wote?

Mabaharia wangelazimishwa kufanya nini?
Mawimbi yalikuwa madogo?
Papa wangefanyaje?
Abiria wangefurahi kuwa wapi?
Tuliamini nini?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 48

LESSON 48


PESA KWA POSTA

1st PERIOD — PERCEPTION DRILL — LESSON 48

Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on the 'NGALI' tense.

a. Ungalipenda.
Ungaliona.
Ungalituma.
Ungalilipa.
Ungaliweza.

b. Ningalitaka.
Ningalikuomba.
Ningalipenda.
Ningalilipa.
Ningalitoa.

c. Tungalifika.
Tungalitembea.
Tungalichoka.
Tungalifuata.
Tungalipenda.

d. Angaliniomba.
Angalinijibu.
Angalielimishwa.
Angalimsaidia.
Angalimpa.

e. Mngalipenda.
Mngaliandika.
Mngalisoma.
Mngalikula.
Mngalikunywa.

f. Wangalipigana.
Wangalishambulia.
Wangalipata.
Wangalirudi.
Wangalielimishwa.

2. Semantic drills.

a. Tuma simu.
Tuma barua.
Tuma mtoto.

b. Kumtumia mtu barua.
Kutumia silaha.
Kutumia chombo.

c. Aliniomba msaada.
Alimwomba Mungu.
Alituomba pesa.

d. Karani wa duka.
Karani wa posta.
Karani wa afisi hii.

e. Nimechoka.
Nitapumzika.

f. Gharama ya simu.
Gharama ya safari.

g. Aliniuliza.
Nilimjibu.

h. Amepata elimu.
Ameelimishwa.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Would you have liked to send a cablegram from Nairobi to America?

   Yes, I would have liked to send my brother a cable.

2. Would you have had trouble filling in a form for the cable?

   I would have requested your help to send this cable.

3. Would you have sent money by wire as well?

   Yes, my brother has trouble as he lacks money.

4. Would you have sent the wire on day rates?

   No, I would have liked it to go as a night letter.

5. By what way would we have reached the cable office?

   We would have walked, it is only a distance of 4 miles.

6. We would have tired walking.

   We would have taken a short cut and would not have tired much.

7. Would you have paid the cable expenses yourself?

   Yes, I'd have paid even at a shilling a word.

8. Where would you have gotten money?

   I would have drawn from savings at the post office.

LESSON 48


1
??
V,
2
??
3
?? ££
!!
V,
4
??
£ sh
X,
BARUA YA USIKU
5.
?
POSTA
<---Maili 4--->
6
7
??
£ sh.
V,
sh. . sh.
8
?
£ sh.
AKIBA YA POSTA
£
sh.

1. Ungalipenda kutuma simu kutoka Nairobi kwenda Amerika?

   Ndio, ningalitaka kumtumia ndugu yangu simu.

2. Ungaliona shida kujaza kartasi za simu?

   Ningalikuomba msaada kutuma simu hiyo.

3. Ungalituma pesa kwa simu vilevile?

   Ndio, ndugu yangu ana taabu ya pesa siku hizi.

4. Ungalituma simu kwa bei ya mchana?

   La, ningalipenda simu iende kama barua ya usiku.

5. Tungalifika afisi ya simu kwa njia gani?

   Tungalitembea, ni mwendo wa maili nne tu.

6. Tungalichoka kwenda kwa miguu?

   Tungalifuata njia fupi hatungalichoka sana.

7. Ungalilipa gharama ya simu mwenyewe?

   Ndio, ningalilipa hata ingalikuwa shilingi kwa kila neno.

8. Ungalipata wapi pesa?

   Ningalitoa pesa kutoka akiba yangu ya posta.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Angalipenda kutuma simu angalifaulu.
Angalipenda kutuma simu angalifaulu.

tamani, jua, taka, kumbuka.

b. Ningalimwonya arudi hapa angalikataa.
Ningalimwonya arudi hapa angalikataa.

ambia, uliza, taka, amrisha.

c. Ungalikata tamaa ungalipotea.
Ungalikata tamaa ungalipotea.

chelewa, umia, gongwa, karibia.

d. Tungalitembea tungalichoka sana.
Tungalitembea tungalichoka sana.

fanya kazi, rudi, fuatana, kazana.

e. Wangaliona shida wangaliumia.
Wangaliona shida wangaliumia.

gongana, ogelea, gongwa, kimbia.

f. Mngalituma simu mngalilipa pesa.
Mngalituma simu mngalilipa pesa.

ingia, chelewa, onekana, hudhuria.

2. Substitution Drill

a. Usingetuma simu
---------- ---- usingenipata.
Usingetuma simu usingenipata.

fanya haraka, vumilia, ngojea, amini.

b. Asingeomba msaada
---------- ------ asingefaulu.
Asingeomba msaada asingefaulu.

fanya kazi, weka akiba, fahamu Kiswahili.

c. Nisingetembea
------------- nisingefika huko.
Nisingetembea nisingefika huko.

kazana, kimbia, jifunza, omba msaada.

d. Asingaliomba ruhusa
------------ ------ asingalifika hapa.
Asingaliomba ruhusa asingalifika hapa.

uliza, kazana, kimbia, toroka, burudika.

e. Usingalinifuata
--------------- usingalipata taabu.
Usingalinifuata usingalipata taabu.

ita, uliza, ambia, karibia.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the question and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Ungalitaka kutuma simu jana?
2nd: Ndio, ningalitaka.

jaribu, weza, faulu, tamani.

b. 1st: Angalifika bila kufanya bidii?
2nd: Najua angalifika bila kufanya bidii.

faulu, fanya kazi. ondoka, hudhuria mkutano.

c. 1st: Wangalikuona wangalikupiga?
2nd: Wangalinipiga sana.

umiza, saidia, tuma, salimia.

d. 1st: Mngalifaulu mngalifurahi?
2nd: Ndio, tungalifurahi.

ingia, okoka, fika, ondoka.

e. 1st: Tungaliwaona wasingaliondoka?
2nd: Ndio, wasingaliondoka.

saidia, salimia, tambua, fahamu.

5th PERIOD RECOMBINATION DRILL LESSON 48

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Ungeondoka ungewakamata?
Ningeondoka singewakamata.

ona, uliza, tambua, fundisha,

b. Angalijua angalikaa hapa?
Ndio, angalikaa hapa.

ondoka, lala, ishi, fanya kazi.

c. Wangekuambia ungewaamini?
Wangeniambia singewaamini.

lipa, umiza, fuata, penda.

d. Mngaliokoka mngalilalamika?
Tungaliokoka tusingalilalamika.

rudi hapa, endelea mbele, kata tamaa.

e. Wangalituma simu ingalifika?
Wangalituma simu ingalifika.

potea, enda, kupendeza, waonya.

f. Tungalitazama tungalielewa?
Ndio, tungalielewa.

fahamu, amini, umia.

g. Angalikuruhusu ungalimwacha?
Angaliniruhusu nisingalimwacha.

ambia, uliza, fukuza, fuata.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Juma angalipenda kutuma simu kutoka Nairobi kwa ndugu yake kule Amerika. Juma ni mkulima na hakuelimishwa sana. Hivyo hangaliweza kujaza karatasi ya simu vizuri. Lakini rafiki yake aliyeelimishwa angalimsaidia. Juma alipata barua kutoka ndugu yake anayesoma katika skuli kubwa kule Amerika. Gharama ni kubwa sana na hivi alipata taabu ya pesa. Juma aliuza mavuno yake na angalipenda kumsaidia. Aliweka pesa chache akiba kule posta.

Walipofika posta karani aliwauliza kama wangependa kutuma simu kwa bei ya mchana au kama barua ya usiku. Juma alijibu kwamba angalituma simu kama barua ya usiku sababu ni rahisi zaidi. Vilevile angalipenda kutuma pesa kwa simu na angalitoa pesa kutoka akiba yake kule posta. Karani alitengeneza kila kitu, na simu, hata na pesa, ilifika Amerika salama.

Step 2. Questions based on the above narration:

Ndugu ya Juma anakaa wapi?
Juma angalituma simu kutoka wapi?

Juma anafanya kazi gani?
Alijua kusoma na kuandika vizuri?
Nani angalimsaidia kujaza karatasi?

Ndugu aliyejifunza Amerika alimwandikia nini?
Gharama ya skuli ni kubwa?
Juma alipata faida alipouza mavuno?
Aliweka pesa zake wapi?
Juma angalituma pesa vilevile?

Simu kwa bei ya mchana ni ghali zaidi?
Kama barua ya usiku simu ni rahisi zaidi?
Juma angalipata wapi pesa?
Karani alimsaidia vizuri?
Simu na pesa zilifika salama?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 49

LESSON 49



Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on the 'KI' tense.

a. Nikiangalia nitaona.
Nikipita nitafika.
Nikiweza nitafanya.
Nikipenda nitampa.

b. Nikiwaita watakuja.
Nikiwauliza watajibu.
Nikikariri watafahamu.
Nikiwaonyesha watajua.

c. Tukipoteza wakati tutachelewa.
Tukishambulia tutafaulu kutoka.
Tukiwaingilia upande wa kulia.
Tukiwaingilia upande wa kushoto.

d. Mkiangalia mtaona.
Mkipigana mtashinda.
Mkivuka mto mtaonekana.
Mkipanga sehemu ni bora.

e. Ukipenda kula, nenda kula.
Ukitaka pesa, fanya kazi.
Ukiondoka tutakufuata.
Ukichelewa utamkosa.

2. Semantic drills.

a. Mkono wa kulia.
Upande wa kulia.
Elekea kulia.

b. Mguu wa kushoto.
Upande wa kushoto.
Elekea kushoto.

c. Kushambulia boma.
Kuingilia boma.
Kuteka boma.

d. Njia yenye miamba.
Njia yenye matope.
Njia yenye hatari.

e. Mto katika bonde.
Msitu katika bonde.
Boma katika bonde.

f. Fanya kwa akili !
Gawanya kwa akili !
Shambulia kwa akili !

g. Gawanyeni sehemu mbili.
Sehemu ya kwanza.
Sehemu ya pili.

h. Watavuka kwa daraja.
Watavuka kwa mitumbwi.
Watavuka kwa chelezo.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Captain! We must make plans for an attack today.

   Very well, Major! If I call the officers they'll come at once.

2. Blow the whistle, if we lose time we'll be late.

   We've arrived, Sir! If you issue orders we'll listen.

3. If you look at this map you'll see a big valley here.

   Yes, and the fort of the enemy is here on the bank of the river.

4. Correct, if we attack intelligently we'll succeed in capturing the fort.

   How should we divide our unit?

5. If we divide it into two sections it will be best.

   If we enter enemy lines from the left is that best?

6. No, there we would be compelled to go through much mud.

   Shall we go in from the right then?

7. O.K., there we would get cover among the big rocks.

   If we cross the river on a raft will we be seen?

8. No, it will be difficult to spot us because of camouflage.

   We should go over this again so we won't forget.

LESSON 49


1
+++
Meja
2
3
&
4
?
5
+++
kushoto
??
+++
6
X,
??
kulia
7
8
X,
!!

1. Kapteni! Lazima tufanye mpango kwa shambulio leo.

   Vema, Meja! Nikiwaita maofisa watakuja sasa hivi.

2. Piga filimbi, tukipoteza wakati tutachelewa.

   Tumefika, Effendi! Ukitoa amri tutasikiliza.

3. Mkiangalia ramani hii mtaona bonde kubwa hapa.

   Ndio, na boma la adui ni hapa ukingoni mwa mto.

4. Kweli, tukishambulia kwa akili tutafaulu kuteka boma.

   Tugawanye jeshi sehemu ngapi?

5. Tukipanga sehemu mbili ni bora zaidi.

   Tukiwaingilia adui upande wa kushoto si bora?

6. La, hapo tungelazimiwa kupitia katika matope mengi.

   Tungewaingilia upande wa kulia basi.

7. Vema, hapo tungepata maficho katika miamba mirefu.

   Tukivuka mto kwa chelezo tutaonekana?

8. La, ni vigumu kutuvumbua sababu ya kamuflaji.

   Tungekariri mpango huu tena ili tusisahau.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Nikipiga filimbi watatoroka.
Nikipiga filimbi watatoroka.

lala, chelewa, karibia, ondoka.

b. Ukitoa amri tutasikiliza.
Ukitoa amri tutasikiliza.

ongea, sema, penda, keti.

c. Akiamini nitafurahi.
Akiamini nitafurahi.

tangulia, onekana, kumbuka, piga filimbi.

d. Wakitutisha tutawaumiza.
Wakitutisha tutawaumiza.

danganya, sukuma, fuata, gonga.

e. Mkinifuata mtachelewa.
Mkinifuata mtachelewa.

amini, ngojea, karibia.

f. Tukihudhuria atatuona.
Tukihudhuria atatuona.

karibia, kutanika, fuatana, chelewa.

2. Substitution Drill

a. Ukitoroka
--------- tutakuonya.
Ukitoroka tutakuonya.

ondoka, kimbia, keti, lala.

b. Akiniita
-------- nitakwenda.
Akiniita nitakwenda.

onya, pendeza, tangulia, ambia.

c. Nikimtaja
--------- ataniumiza.
Nikimtaja ataniumiza.

gonga, vizia, fuata, shtaki.

d. Wakituonya
---------- tutarudi.
Wakituonya tutarudi.

ita, fuata, vizia, lipa.

e. Tukiwalazimisha
--------------- watakubali.
Tukiwalazimisha watakubali.

shambulia, uliza, onya, ingilia.

Step 2. Language lab session (if applicable)

This will be a 20 to 30 minute session in the lab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue.

b. Pattern drill.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

Step 1. Sound production drills. 5-10 min. with structural target elements reinforced.

Step 2. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 3. Patterned response drill.

Instructions: In the first part of the drill the teacher asks the question and the student gives the answers.
In the second part the teacher cues one student who asks the question. Then the teacher selects another student to answer the question.

a. 1st: Tukiwashambulia watatoroka?
2nd: Watatoroka tukiwashambulia.

ona, ita, fuata, onya.

b. 1st: Mkituvumbua mtatuumiza?
2nd: Ndio, tutawaumizeni.

shambulia, ingilia, vizia, fuata.

c. 1st: Wakitawanyika tutawafuata?
2nd: Wakitawanyika hatutawafuata.

toroka, vuka mto, shambulia, piga filimbi.

d. 1st: Ukilazimishwa utajifunza?
2nd: Sitajifunza nikilazimishwa.

amrishwa, burudika, chelewa, choka.

e. 1st: Akisikiliza atafahamu?
2nd: Ndio, atafahamu.

ambiwa, ona, soma, jifunza.

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Nikikuambia utatosheka?
Ukiniambia sitatosheka.

lipa, pa, linda, fundisha.

b. Ukimwangalia atafahamu?
Hatafahamu nikimwangalia.

fundisha, eleza, onyesha, amuru.

c. Akituamini tutamwongoza?
Tutamwongoza akituamini.

uliza, onyesha, pendeza, shtaki.

d. Wakikuuliza utawaeleza?
Sitawaeleza wakiniuliza.

kamata, teka, funga, ruhusu.

e. Mkiwakomesha watakata tamaa?
Hawatakata tamaa tukiwakomesha.

fukuza, vumbua, shambulia, tambua.

f. Tukimtuma ataondoka?
Hataondoka tukimtuma.

eleza, fuata, acha, onyesha.

g. Ukipenda utaondoka?
Ndio, nikipenda nitaondoka.

maliza, kumbuka, elewa, umia.

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Meja alimwita Kapteni na alimwambia awaite maofisa kusikiliza amri zake. Kapteni aliona akipiga filimbi, wote watasikia na watakuja haraka. Meja aliona ni lazima kufanya mpango kwa kushambulia leo.

Wakiangalia ramani wataweza kuona bonde kubwa na mto. Ukingoni mwa mto ni boma la adui. Wakishambulia boma kwa akili wangefaulu kuteka boma. Hivi wakigawanya jeshi sehemu mbili ingekuwa bora. Wakiingilia adui upande wa kushoto si vizuri sababu ya matope mengi. Lakini wakiingilia upande wa kulia wangefaulu na wangepata maficho katika miamba mikubwa.

Ofisa mmoja aliogopa wataonekana wakivuka mto kwa chelezo, lakini wakitumia kamuflaji (vidanganya macho) adui hatawavumbua. Wote waliomba Meja kueleza tena na kukariri mpango wa mashambulio ili wasisahau.

Step 2. Questions based on the above narration:

Nani alimwita Kapteni?
Alitaka amwite nani tena?

Kapteni alitumia njia gani kuwaita?
Meja alitaka kufanya mpango gani?
Wakisikia filimbi watakuja upesi?

Katika ramani waliona nini?
Boma la adui lilikuwa wapi?
Wangeweza kuteka boma lile?
Walitaka kugawanya jeshi sehemu ngapi?
Upande wa kushoto kuna nini?

Wakiingilia upande wa kulia wangefaulu?
Wangepata maficho wapi?
Ofisa mmoja aliogopa nini?
Walitaka kuvuka mto kwa njia gani?
Maofisa waliomba nini?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

SWAHILI 12 WEEKS COURSE

LESSON 50


2

Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on the 'A' tense.

a. Twende mgahawani.
Twataka chakula.
Twapenda pombe.

b. Naja, mabwana.
Nafurahi kukaa hapa.
Nala hapa siku zote.

c. Apenda kuagiza chai.
Apata bakshishi.
Aleta machupa mawili.

d. Wapenda kitoweo?
Wapenda bia?
Wala mboga?

2. Drill on the conditional tense.

a. Mngependa kuagiza?
Mngependa kunywa nini?
Mngekunywa kahawa?

b. Tungependa kitoweo.
Tungekula mchuzi wa binzari.
Tungeagiza ndizi iliyopikwa.

c. Ungelipa gharama?
Ungempa bakshishi?
Ungepata bia?

d. Angeleta chakula cha mwisho?
Angependa nyama ya kondoo?
Angerudi mgahawani tena?

3. Semantic drills.

a. Unakaa katika hoteli?
Unaingia katika hoteli?

b. Unakwenda mgahawani?
Unakula katika mgahawa?

c. Mtumishi analeta chakula.
Mwite mtumishi alete hesabu.

d. Mgeni anaagiza kitoweo.
Mabwana wanapenda kitoweo.

e. Ndizi ni mboga.
Nyanya ni mboga.

f. Mchuzi wa nyanya.
Mchuzi wa binzari.

g. Matunda mabivu.
Ndizi mbivu.

h. Mkate na siagi.
Anatia siagi juu ya mkate.

i. Mapambo mazuri.
Mapambo malidadi.

j. Mtumishi anapata bakshishi.
Alipata bakshishi nzuri.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Shall we go to a café or hotel?

   This café will do.

2. Hi, waiter, we want to order food.

   I'm coming, gentlemen, what would you like to order?

3. We'd like a mutton stew.

   Would you like it with curry gravy?

4. Yes, and for vegetable we'd like bananas and tomatoes.

   And what for dessert?

5. Some ripe fruit will satisfy us.

   And what would you like to drink, tea or coffee?

6. Bring two bottles of beer.

   O.K., you'll get it all quickly, also bread and butter.

7. This café is pleasing in its cleanliness.

   All utensils are new and furnishings are decorative.

8. Put all expenses on one account.

   O.K. Please come again! Thanks for the tip.

LESSON 50


1
??
HOTELI
MGAHAWA
MGAHAWA
2
!..
Mabwana,
?
3
??
BINZARI
4
Mboga
&
&?
5
&?
CHAI
KAHAWA
6
ok
7
&
8
ok
!

1. Twende mgahawani au hoteli?

Mgahawa huu utafaa.

2. Ee, mtumishi, twataka kuagiza chakula.

Naja, mabwana, mngependa kuagiza nini?

3. Tungependa kitoweo cha nyama ya kondoo.

Mngependa mchuzi wa binzari vilevile?

4. Ndio, na kwa mboga tungependa ndizi na nyanya.

Na kwa chakula cha mwisho, je?

5. Matunda mabivu yatatutoshea.

Na mngependa kunywa nini, chai au kahawa?

6. Lete machupa mawili ya pombe (bia).

Vema, mtapata yote upesi, hata mkate na siagi.

7. Mgahawa huu unapendeza kwa usafi.

Vyombo vyote ni vipya na mapambo ni malidadi.

8. Andika gharama zote juu ya hesabu moja.

Vema. Tafadhali rudini tena. Asante kwa bakshishi.

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Mngesafisha migahawa tungetosheka.
Mngesafisha migahawa tungetosheka.

fagia, tafuta, tunza, pata.

b. Twataka kitoweo cha nyama.
Twataka kitoweo cha nyama.

nunua, uza, tengeneza, leta.

c. Mkiniamini mtaokoka.
Mkiniamini mtaokoka.

